Nipashe
Jumamosi Machi 7, 2020 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0580173
The Guardian digital
www.ippmedia.com
nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710



## Bibi wa miaka 90 asimulia ruzuku Tasaf ilivyobadilisha maisha yake

UKUR




UKURASA 13

# CCM: Tunatumia dola kubaki madarakani

**DK. BASHIRU** asema hata wapinzani wakiingia watafanya hivyo, ataka wabunge, madiwani walioboronga waanze kufungasha... *Endelea ukurasa wa 2*



Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally.

## WANAFUNZI WAKUMBWA NA UGONJWA WA AJABU

UKURASA 4

# Vyama vya siasa hatarini kufutwa kabla uchaguzi

UKURASA 3



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play App Store

MICHEZO SIMBA, YANGA ZASUBIRI MUDA UK. 32

MAONI, KATUNI UK.6



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally (kulia), akifurahia jambo na wahariri na viongozi waandamizi wa kampuni ya The Guardian Ltd, inayochapisha magazeti ya The Guardian na Nipashe, alipotembelea ofisi za kampuni hiyo, eneo la Viwandani, Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# CCM: Tunatumia dola kubaki madarakani

**Na Waandishi Wetu**

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ali, amekiri chama chake kuitumia dola kuhakikisha kinabaki madarakani.

Amesema kama chama chochote kinachoongoza serikali kitashindwa kutumia dola kubaki madarakani, utakuwa uzembe wa chama chenyewe.

Kwa kulitambua hilo, Dk. Bashiru amesema CCM imekuwa ikitumia dola kujihakikishia ushindi wakati wa uchaguzi na mwaka huu wamepanga "kuitumia dola kweli kweli".

Lakini, kiongozi huyo wa CCM akaonya kuwa chama kinachoongoza serikali, hakipaswi kuitumia dola kunyanyasa wapinzani wake.

Dk. Bashiru aliyasema hayo katika mahojiano maalum na vyombo vya habari vya IPP alivyovitembelea jijini Dar es Salaam jana.

"Ukishakuwa chama tawala, kuna dhana inaitwa nafuu ya mwenye madaraka. Ukishindwa kutumia nafuu hiyo, utakuwa kama KANU (chama tawala cha zamani cha Kenya), iliposhindwa kutumia nafuu hiyo, haikuwahi kurudi madarakani au UNIP ya Zambia.

"Unashika dola halafu unatumia dola kubaki madarakani. Akitokea mtu mwenye busara zaidi, akakwambia usitumie dola, ukamsikiliza, siku ukishatoka hurudi!

"Hata kwenye kazi, kazi inatafuta kazi. Kwa hiyo, aliye na dola anatumia dola hiyo kubaki madarakani. Ukweli hata Chadema ikiingia madarakani, kuiondoa kwenye dola itakuwa ni uzembe wake, kwa sababu ana nafuu na faida ya kuwa na dola.

"Kinachotakiwa usitumie dola vibaya kunyanyasa wapinzani wako. Wanaosubiri sisi (CCM) tulegelege kutotumia dola kubaki kwenye dola, watasubiri sana. Huo ndio ukweli, si wa Tanzania, si wa CCM, hata (Donald) Trump (Rais wa Marekani) kumwondoa leo ni ngumu," alisema.

Alipotakiwa kutoa ufafanuzi kuhusu kauli yake hiyo, Dk. Bashiru alisema: "Watu wakisema unatumia dola, wanadhani unakwenda kuiba, dola ni chombo cha wananchi, kutumia dola ni kutumia wananchi waliokukabidhi dola ili wakubakize kwenye dola, hii ndiyo maana yake tu.

"Hawa wananchi ambao tumeshirikiana wote kutafuta maji, kujenga miundombinu ya barabara kwa kodi zao, hakuna chombo kinachoweza kukusanya kodi ambacho si dola, ndiyo moja ya sifa, sifa kubwa ya dola ni kukusanya kodi, tutatumia kodi za wananchi.

"Ndiyo matumizi ya dola, tutatumia vyombo vya ulinzi na usalama kuwahakikishia wananchi wako salama, ndiyo matumizi ya dola.

"Sasa, wewe ukiwa na dola halafu wahuni wanakwenda Rufiji na Kibiti, si unakumbuka kulikuwa hakupitiki? Tulitumia dola kulinda usalama wa watu. Nimepita mara nyingi wakati mwingine ninashuka kula kuku wa kuchemsha, hayo ndiyo matumizi ya dola ninayosema."

Dk. Bashiru alisema wanatumia dola kwa sababu wamekabidhiwa dhamana kutumia vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha usalama upo.

"Kutumia vyombo vya ulinzi na usalama kukabiliana na rushwa, tumevitumia kuwatisha wala rushwa, sasa hayo matumizi mabaya? Tutaitumia kweli kweli.

"Matumizi ya dola ni kuwatumia wananchi wenye dola kwa kuwa dola ni mali ya wananchi, sisi tumekabidhiwa dhamana ya kuiendesha, tukiiendesha vizuri wananchi watatuamini zaidi, tukiiendesha vibaya, watatuadhibu, wanampa mtu mwingine. Hata hao wengine wanatafuta dola.

"Faida tuliyo nayo tuna dola, wengine wanatafuta, mwenye dola akiishika vizuri, akaitumia vizuri na kufanya yale iliyoahidi, akatumia vizuri kujengea imani wapigakura, hawabadilishi ile dola kumpa mtu mwingine, hii ndiyo faida ya kuwa na dola.

"Mwaka huu kuna uchaguzi, tunakwenda kuomba, yaani tutapiga magoti tukiwa na maelezo mnajua tuliahidi hiki, tumefanya hivi, mmetupa kodi zenu tumefanya haya. Kwa hiyo watu wasitafsiri vibaya, lakini huwezi kuzuia tafsiri kwa kuwa hii ni dhana ya kifalsafa kidogo.

"Mtu anaweza kutumia maneno haya niliyoyasema akatafsiri vingine, maana yake ni hiyo, tutatumia dola kodi, taasisi za serikali kutekeleza ilani, tutatekeleza ahadi na kufika Oktoba, tutakuwa kwenye nafuu zaidi na faida zaidi kubaki madarakani," alifafanua.

**KIFO CHA UPINZANI**

Alipoulizwa kuhusu madai ya kuwapo mkakati wa chama chake kuhakikisha kinaua upinzani nchini, Dk. Bashiru alisema hakuna dhamira hiyo, lakini kama kuna vyama vitakufa, CCM haiwezi kuzuia.

"Hatuna mpango wa kuzuia kifo, siyo kazi yetu kuzuia kifo cha chama, ni jukumu la chama kutokufa, mtu atakayekaa barabarani kusababisha chama kife kwa kushindwa ni halali yangu, na hili ni jukumu la vyama vyote vilivyosajiliwa kubaki hai, siyo jukumu la CCM kuvilea vyama visife, kifo kibaya cha chama huanza mapema.

"Ni kama ugonjwa wa kichwa, huanza taratibu, maumivu ya kichwa huanza polepole, na kifo cha chama huanza polepole kwa kushindwa, kifo cha kisiasa siyo kifo cha watu na katika siasa kuna kufa na kuzaliwa, vipo vilivyokufa, vipo vinachechemea, vingine haviwezi kufa, navijua," alisema.

Dk. Bashiru pia alitolea ufafanuzi madai ya CCM kununua wanachama kutoka vyama vya upinzani, akisema hakuna anayenunuliwa na kwamba wanaotoka upinzani ni 'watamu kweli' na matarajio yao ni kupokea wengine wengi zaidi kipindi hiki.

"Sijawahi kuona mavuno mazuri kama ya mwaka huu na mwaka jana na shughuli inaendelea, kama huo ndiyo mwelekeo wa vyama vya upinzani kufa, vijifunze namna ya kutunza wanachama wao," alitamba.

**MCHUJO MKALI CCM**

Katika mahojiano hayo, Dk. Bashiru pia alidokeza kuwapo mchujo mkali ndani ya chama kuwapata wagombea wa nafasi za udiwani na ubunge katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu na kuweka wazi kuwa mgombea wao wa urais mwaka huu ni Dk. John Magufuli.

Alisema kuna vigezo kadhaa vitakavyozingatiwa ikiwa ni pamoja na kufuatilia nyendo za wanachama wao ambao tayari wameshaanza kupitapita na kupenyeza fedha kwa miamala ya simu ili kupita kwenye kura za maoni.

"Ninawatahadharisha, uteuzi siyo kura za maoni peke yake, ni kura za maoni na mjadala wa jina kwa jina kuhusu sifa za aliyeshinda na kukubalika kwa wananchi, hatutafuti wagombea wa CCM, tunatafuta wagombea wa CCM watakaopigiwa kura na wana CCM na wasiyo wana CCM na mwisho vikao ndivyo vinateua," alisema.

Dk. Bashiru alisema kila mwana CCM ana haki ya kugombea uongozi, lakini hana haki ya kuteuliwa kwa sababu uamuzi wa kuteua ni wa vikao na hakuna atakayeteuliwa kuwania ubunge na udiwani bila kuangalia rekodi yake ya utendaji na mahudhurio yake kwenye vikao vya Bunge na mabaraza.

"Hakuna uteuzi wa bure, wapo wanaojihangaisha kuzungumza na wapigakura wakidhani wakimalizana nao kwenye kura za maoni, wamepata uteuzi, tutazingatia kura za maoni, na kwenda kwenye kumbukumbu zako ulisema nini, uliahidi nini na umetekeleza nini," alionya.

Dk. Bashiru pia alizungumzia maandalizi ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM mwaka huu, akisema imejikita katika vipaumbele vitatu ambavyo ni kilimo, maji pamoja na ulinzi na usalama.

**UKAWA TISHIO**

Mhadhiri huyo wa zamani wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), pia alikiri kuwa kuungana kwa baadhi ya vyama vya siasa katika kile kilichoitwa Umoja wa Katiba ya Wananchi (Ukawa), kulikuwa tishio kwa CCM katika uchaguzi mkuu uliopita.

Alisema hilo lilijidhihirisha kwenye idadi ya kura ambazo CCM ilizipata kwa nafasi ya urais, akibainisha kuwa ilikuwa mara ya kwanza mgombea wao kushinda kwa kura chache.

Mtaalamu huyo wa sayansi ya siasa alisema Ukawa pia ulisababisha CCM kupoteza majimbo mengi zaidi tangu kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi nchini.

"Rais John Magufuli alipata kura ambazo mgombea wa CCM hajawahi kuzipata katika mfumo wa vyama vingi -- asilimia 58 na mgombea wetu (alikuwa) hajawahi kutofikia asilimia 60, Rais mstaafu Jakaya Kikwete wakati anaingia alifikia asilimia 80," alifafanua.

Dk. Bashiru pia alitoa ufafanuzi kuhusu kauli yake kwamba mchakato wa Katiba Mpya ni kiporo kilichochacha, akisema Ukawa ulioaminiwa na wananchi umesambaratika.

"Ndiyo maana nakiita kiporo kilichochacha, Ukawa iko wapi? Wanaweza kuingia na ajenda hiyo mwaka huu? Wanaweza kuaminika mwaka huu? Walikuwa wanatafuta Katiba Mpya kweli? Haijapatikana wamesambaratika...

"Kumbe ilikuwa ni geresha, ilikuwa ni kuteka mchakato wa Katiba Mpya kutafuta Ikulu, Ikulu haikupatikana, Ukawa imesambaratika. Kuwa na wanasiasa wa namna hiyo wa kuwavuta wananchi kutafuta jambo jema na kuwaacha solemba, nacho ni kiporo kilichochacha.

"Sasa, unataka kuumwa matumbo kula kiporo cha namna hiyo? Hatujamaliza matatizo ya Corona, tuingie kwenye kuumwa matumbo? Rais Magufuli akasema 'hatuwezi kuwa na siasa za kinafiki, watu wanatafuta Ikulu kwa kisingizio cha Katiba Mpya'", alisema.

**UPINZANI KUITWA IKULU**

Dk. Bashiru pia alimpongeza Rais Magufuli kwa kuendelea kukutana na Watanzania wa makundi mbalimbali Ikulu, akikumbusha kuwa amefanya hivyo kwa wafanyabiashara, wenye ulemavu na makundi mengi ambayo hukutana na wasaidizi wake.

"Ameshatuelekeza tukutane na makundi ya wawakilishi wote, anakutana na mabalozi, hata viongozi wa upinzani wana haki ya kukutana naye Ikulu, ndiye pekee ameifanya Ikulu ionekane ni ya Watanzania.

"Kama hiyo ndiyo inatajwa ni kujenga maridhiano, ni mkakati mzuri lakini siyo ile ya mtazamo wa kisiasa, bali kwa mtazamo wa kitaifa, Ikulu ni ya Watanzania wote na kila mmoja anaweza kukutana na Rais Ikulu," alisema.

**Imeandikwa na Romana Mallya, Salome Kitomari na Enock Charles.**

HABARI KITAIFA

# Vyama vya siasa kupigwa panga

**Na Mary Geofrey**

MSAJILI wa Vyama vya Siasa nchini, Jaji Francis Mutungi, amesema watafanya uhakiki wa vyama vya siasa ili kuangalia uhalali wao kabla ya kushiriki uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Amesema katika uhakiki huo, vyama vya siasa ambayo vitakuwa havijakidhi vigezo na matakwa ya ofisi yake, vitakuwa vimekosa sifa ya kushiriki katika uchaguzi huo unaojumuisha nafasi za udiwani, ubunge na urais.

Jaji Mutungi aliyasema hayo katika mahojiano maalum na Kituo cha Luninga cha ITV, akibainisha kuwa tayari wameshaviandikia barua vyama vyote kupitia kwa makatibu wake kuwaeleza kuwa kutakuwa na uhakiki kuanzia Machi 10 mwaka huu.

Alisema uhakiki utahusisha vyama vyote 19 vyenye usajili wa kudumu kwa lengo la kuhakikisha uhai wao katika vyama na ili washiriki wote kwenye uchaguzi mkuu.

"Kazi ya uhakiki ni moja ya majukumu yanayofanywa na Ofisi ya Msajili na kazi ya chama ni kutunza uhalali wake, kuhakikisha kinakuwa hai, hivyo tunapofanya uhakiki, ni kujiridhisha 'je, kuna vyama ambavyo vimeshapoteza sifa za kuendelea kuwa vyama vya siasa?'", alisema.

Kiongozi huyo alisema chama kitakachobainika kuwa kimepoteza sifa za kulinda usajili wake kwa kawaida, hakitapata nafasi ya kushiriki katika uchaguzi huo.

"Tumefanya hivyo mapema ili kutoa nafasi kwa vyama ambavyo havijatimiza matakwa ya tume, basi zirekebishe hizo dosari ili viwe na uhalali wa kushiriki kwenye uchaguzi mkuu unaokuja," alisema.

Jaji Mutungi alisema wameshaandaa ratiba ya kuvitembelea vyama hivyo na vyama vyote vina taarifa ya ziara hiyo na kwa kuanza, watakutana na makatibu watendaji wa vyama vyote kuzungumza nao kuhusu uhakiki huo.

Alisema kuanzia Machi 12 mwaka huu, wataanza kutembelea vyama kwa mujibu wa ratiba waliyojiwekea.

Kuhusu hali ya kisiasa nchini, Jaji Mutungi alisema vyama vingi vya siasa vimekuwa na utulivu na kufuata sheria na kuvitaka kuendelea kudumisha utii wa sheria bila shuruti wakati wa kuelekea uchaguzi mkuu.

"Siyo tu wanasiasa, na wananchi wote wakifuata sheria za nchi zilizowekwa, nchi itaenda vizuri bila kuwapo na misuguano yoyote," alisema.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akikabidhi tuzo kwa Meneja Rasilimali Watu wa TBL, GoodLuck Lusingu, kutokana na mchango wa kampuni hiyo, kutoa ajira na kuendeleza vipaji wakati wa mkutano wa Mawaziri na wadau wa utatu wa sekta ya ajira wa SADC, unaoendelea, jijini Dar es Salaam juzi. Kushoto ni Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Ajira na Watu wenye Ulemavu ), Mh. Jenista Mhagama. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Bibi wa miaka 90 asimulia Tasaf kubadili maisha yake

**Na Mwandishi Wetu, CHUNYA**

BIBI mwenye umri wa miaka 90, Rozina Mwambogo, mkazi wa kijiji cha Mapogoro, Chunya mkoani Mbeya, ameelezea alivyoboresha maisha yake kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini.

Kupitia mpango huo unaotekelezwa na Mfuko wa maendeleo ya Jamii (Tasaf), Mwambogo amesema ameboresha maisha yake kwa kujenga nyumba ya kuishi, kujishughulisha na kilimo na mazao ya chakula ikiwa ni pamoja na kufuga nguruwe.

Alitoa ushuhuda huo juzi wakati wa ziara ya kikazi ya Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa, wilayani Chunya yenye lengo la kukagua utekelezaji wa mpango huo mkoani Mbeya.

Bibi huyo alisema kabla ya kuingizwa kwenye mpango, hali ya maisha yake ilikuwa duni kupindukia kwa kuwa hakuwa na kipato cha kumwezesha kupata mahitaji muhimu ya kila siku kama chakula na mavazi.

Kutokana na mabadiliko hayo kimaisha, alisema malengo yake ya baadaye ni kuboresha zaidi maisha yake kwa kuongeza idadi ya nguruwe na kuku na kuongeza uzalishaji wa mazao shambani, hasa ya chakula.

Aidha, Mwambogo aliishukuru Serikali kwa kuendelea kuwajali wanyonge na kuwasaidia kupitia Tasaf.

Mwajelwa alimweleza Mwambogo kuwa serikali inazijali na kuzithamini kaya zote maskini nchini ndiyo maana inatoa ruzuku kupitia Tasaf, lengo likiwa kuzikwamua katika lindi la umaskini.

Alisema ziara yake ya kikazi ya kumtembelea bibi hiyo ni sehemu ya kumuunga mkono Rais John Magufuli ambaye amejipambanua kwa vitendo kuwajali wanyonge.

Mwanjelwa alimpongeza Mwambogo kwa kutumia vyema ruzuku anayoipata licha ya umri mkubwa alionao na kutoa wito kwa wananchi, hususani wanufaika wa Tasaf, kutumia vema fedha za miradi ya serikali kama ilivyokusudiwa.

Uhawilishaji wa fedha kwa kaya maskini wilayani Chunya ulianza Julai, 2015 na hadi sasa awamu 23 za malipo zimefanyika na Sh. 7,472,420,000 kimetumika kuwapa walengwa ruzuku.


The Guardian Limited

JOB VACANCY

**The Guardian Limited ,publisher of leading Tanzania newspapers, The Guardian and Nipashe, is looking for motivated and experienced people to fill the position of:**

**CIRCULATION FIELD OFFICER – DAR ES SALAAM**

**Job Purpose:**

To boost copy sales and develop relationships with agents and vendors in the sales channel in the assigned area to meet your set sales targets.

**Main Responsibilities:**

The successful candidates will be responsible for the following key results:

- Work with the agents and vendors in making sure that the business grows and The Guardian Limited publications are available and visible and sold at the set retail prices with optimal return levels.
- Develop and grow more channels of distribution.
- Monitor indicators relating to market arrivals, circulation sales and returns indicators and make appropriate reports to Circulation Supervisor.
- Identify and build rapport with existing and potential customers by communicating the benefits of Selling The Guardian and Nipashe.
- Monitor newspaper distribution and sale trends in particular areas, prepare weekly sales plans and update supervisor on a regular basis.
- Monitor daily performance of TGL brands in your particular areas of operation in comparison to our rival publications and make reports that guide growth strategies.
- Open up new markets in particular areas of operation that will in turn translate into higher sales.
- Attend customer complaints that in one's particular area of operation so as to maintain good customer relations and protect the company's interests.
- Liaise with supervisor in credit control and debt management within particular area of operation.
- Submit daily and weekly reports on progress on activities, including meeting set sales targets.
- Manage debt collection and credit control within one's respective area operation.
- Demonstrate ability to work under minimum supervision.

**Minimum Qualifications and Experience:**

- University Degree in Business Administration/Sales & Marketing or equivalent.
- At least 2 year's relevant working experience.
- Excellent communication skills, computer knowledge, and familiarity with a wide range of newspapers brands.

**MODE OF APPLICATION:**

Apply online via HRO email address: ;**vacancy@guardian.co.tz** by March 13, 2020

NB: Only shortlisted candidates will be contacted.

***The Guardian Limited is an equal opportunity employer.***

615654302

# Majaliwa awaonya wakiukaji maadili

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amesema mtumishi wa umma asiyetaka kufuata maadili ya utumishi na maelekezo ya viongozi wake, hafai kufanya kazi katika serikali ya awamu ya tano.

Majaliwa aliyasema hayo juzi jioni alipokuwa akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Mji wa Korogwe na wananchi kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika katika uwanja wa Chuo cha Ualimu Korogwe akiwa kwenye ziara ya kikazi mkoani Tanga.

Alisema uaminifu na uadilifu ni jambo ambalo linapaswa kupewa kipaumbele na watumishi wa umma nchini, hivyo aliwataka watumishi wasijiingize kwenye mambo ambayo hayana tija katika utumishi wao.

Waziri Mkuu alisema serikali inataka kila mtumishi wa umma nchini awajibike kwa kufanya kazi kwa bidii na kufuata maadili ya kiutumishi na kwamba haitamvumilia mtumishi ambaye ni mwizi, mbadhilifu, mvivu na haitasita kumchukulia hatua.

"Watumishi mnatakiwa muwahudumie wananchi bila ubaguzi wa aliyenacho na asiyekuwa nacho kwa sababu wananchi wote wana haki sawa ya kuhudumiwa, hivyo hakuna sababu ya kuwabagua," alisema.

Pia Waziri Mkuu alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Kissa Kasongwa, kuwasimamia wakuu wa idara katika kupanga ratiba za kwenda vijijini kuwasikiliza wananchi na kushirikiana nao katika kutatua kero zinazowakabili.

Kuhusu upatikanaji wa huduma ya majisafi na salama, Waziri Mkuu alisema serikali ina mikakati mizuri inayolenga kumaliza tatizo hilo na kuwataka wananchi waendelee kuwa na subira wakati suala hilo linashughulikiwa.

Waziri Mkuu alisema serikali kupitia kampeni ya kumtua mama ndoo kichwani, itahakikisha wananchi katika maeneo yote nchini wanapata huduma ya majisafi na salama karibu na makazi yao.

Pia alisema maeneo yote nchini yakiwamo ya Wilaya ya Korogwe, yatasambaziwa umeme kupitia mradi unaotekelezwa na Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Alisema wakati wa usambazaji wa huduma hiyo, wananchi hawatawajibika kulipia gharama za nguzo wala fomu za maombi ya kuunganishiwa umeme kwa kuwa tayari gharama hizo zimeshabebwa na serikali.

"Rais wetu Dk. John Pombe Magufuli anataka kuona kila nyumba ya Mtanzania inapata umeme tena kwa gharama ya sh. 27,000 tu," alisisitiza.

Mbunge wa Korogwe Vijijini, Timotheo Mzava, na mwenzake wa Korogwe Mjini, Mary Chatanda, waliishukuru serikali kwa kuboresha huduma za afya na elimu. Pia waliiomba iwasaidie katika kutatua changamoto za barabara, maji na umeme.

Awali, Waziri Mkuu aliweka jiwe la msingi kwenye mradi wa shamba la ufuta Mkomazi na kujionea miundombinu ya umwagiliaji.

Pia Waziri Mkuu alizindua miradi ya ghala la kuhifadhia nafaka Mombo na kuifungua maktaba ya Chuo cha Ualimu Korogwe.




Mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Kinyerezi, Rahma Seif, akielezea namna ya kujisomea kupitia mfumo wa 'Instant Schools', unaowezesha kupata uelewa mkubwa kwa njia ya mtandao bure kutoka mtandao wa Vodacom, jijini Dar es Salaam, jana. Hii ni hamasa iliyowekwa na Vodacom kuelekea Siku ya Wanawake Duniani kwa mtoto wa kike kupenda masomo ya sayansi yenye kauli mbiu 'I am the face of Tech'. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ugonjwa wa ajabu wawakumba wanafunzi

**Na Stevie Chindiye, Tunduru**

WANAFUNZI 40 wanaosoma katika Shule ya Sekondari ya kiuma, Tunduru mkoani Ruvuma, wamerudishwa nyumbani baada ya kuugua ugonjwa usiofahamika wa kuwafanya wakose nguvu za miguu na mwili kutetemeka.

Taarifa iliyotolewa juzi na Mwenyekiti wa Bodi ya Shule hiyo, Issa Malungusya, ilisema uamuzi huo ulifikiwa baada ya madaktari wa Hospitali ya Misheni ya Kiuma kushindwa kugundua chanzo wa ugonjwa huo unaowatesa wanafunzi hao.

Malungusya alisema baada ya tukio hilo, bodi kwa kushirikiana na walimu wa shule hiyo, walifikia uamuzi wa kuwaita wazazi na walezi wa wanafunzi hao na kuwaruhusu wawachukue ili wakawapatie matibabu na baadaye kuwarejesha shuleni.

Kutokana na hali hiyo, alisema bodi kwa kushirikiana na uongozi wa shule, wamepanga kuwaita wazee wa mila pamoja na viongozi wa dini ili wazungumze nao na kuangalia namna ya kuwaokoa wanafunzi hao na kuwafanya wasome bila hofu wala uoga.

Alisema ugonjwa huo ulianza Machi Mosi, mwaka huu, na kwamba hadi kufikia juzi wanafunzi 40 walikwishaugua ugonjwa huo.

Ugonjwa huo ambao unawakumba watoto wa kike pekee, alisema awali walidhani kuwa huenda chanzo ni kupevuka lakini kilichowashangaza wagonjwa wanaougua ni pamoja na watoto wadogo kabisa ambao bado hawajafikia hatua hiyo.

Ally Mbilijao, mmoja wa wazazi waliokwenda kuwachukua watoto wao, alisema mtoto wake hawezi hata kusimama lakini kutokana na madaktari kushindwa kuwapatia tiba, anafikiria kumpeleka mtoto wake kwa waganga wa tiba asilia ili kuangalia uwezekano wa kumtibu.

Mganga Mkuu wa Wilaya, Dk. Wendy Robert, alipotakiwa kuzungumzi tukio hilo, alisema hana taarifa za tukio hilo na akaahidi kutuma timu ya wataalamu kutoka katika Hospitali ya Wilaya kwenda kujiridhisha juu ya chanzo cha ugonjwa huo.

# Ataka mikakati ya ulinzi wa miundombinu

**Na Julieth Mkireri, KISARAWE**

NAIBU Waziri wa Nishati, Subira Mgalu, amewaagiza wakuu wa mikoa na wilaya nchini, kuweka mikakati madhubuti itakayosaidia kulinda miundombinu ya umeme.

Pia amesema mikakati hiyo itakayoambatana na ulinzi itakuwa msaada kuondoa vitendo hivyo ambavyo vimekuwa vikilisababishia hasara taifa.

Mgalu alitoa agizo hilo jana kutokana na kukithiri kwa matakio ya uhujumu wa miundombinu ya umeme ikiwamo wizi wa mafuta na uharibifu wa Transfoma unaofanywa na watu wasio na nia njema kwa taifa.

Akizungumza akati wa uzinduzi wa ofisi ya Shirika la Umeme Tanzania (Tanesco) katika kata ya Manerumango wilayani Kisarawe, Mgalu alisema ili kukabiliana na uhujumu wa miundombinu ya umeme, kunatakiwa kuwapo mikakati ya kuidhibiti.

"Ni wazi kuwa iko haja kuwapo mikakati ya kudhibiti vitendo hivi ambavyo vimekuwa vinakwamisha azma ya serikali ya kuwapatia umeme wananchi wake kwa wakati na maeneo ambayo tayari wameunganishiwa wanakosa nishati hiyo kutokana na kundi la watu wachache wasiopenda maendeleo," alisema Mgalu.

Akitoa taarifa ya utekelezaji wa miradi ya umeme katika hafla ya uzinduzi wa ofisi hiyo, Meneja wa Tanesco Wilaya ya Kisarawe, Mhandisi Nyanda Busumabu, alielezea mikakati itakayowezesha vijiji vyote wilayani hapa kufikiwa na umeme ifikapo Juni, mwakani.

Busumabu alisema uunganishaji wa nishati hiyo katika maeneo mbalimbali ya Kisarawe utasaidia kufungua wigo wa wawekezaji kuwekeza katika eneo hilo la kimkakati ambalo liko karibu na jiji la Dar es Salam na Hifadhi ya Taifa ya Mwalimu Nyerere (Selous).

Mkuu wa Wilaya ya Kisarawe, Jokate Mwegelo, alisema uwapo wa ofisi hiyo utasaidia kusogeza huduma karibu kwa wananchi na pia itarahisisha upatikanaji wa taarifa pindi linapotokea tatizo na hatimaye kushughulikiwa kwa haraka.

Mmoja wa wakazi wa Manerumango, Idd Konde, aliishukuru serikali kwa uwapo wa ofisi hiyo karibu na wananchi ambayo itawapunguzia kusafiri umbali mrefu kwenda kupata huduma Kisarawe.

# Mchungaji aonya wanawake wanaonyanyasa waume zao

**Na Marco Maduhu, SHINYANGA**

MCHUNGAJI wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Julia Celestine, Dayosisi ya Mashariki mwa Ziwa Victoria, Buzuruga jijini Mwanza, amewataka wanawake kuacha matukio ya ukatili nyumbani mwao kwa kunyanyasa waume.

Akizungumza jana kwenye siku ya maombi ya wanawake duniani, yaliyofanyika mjini hapa kwenye kanisa la Africa Inland Tanzania (AICT) Ngokolo.

Mchungaji huyo aliwataka wanawake wawe watii katika ndoa zao ili kuepusha vifo vya ghafla kwa waume zao na kubaki wajane.

Alisema baadhi ya wanawake wamegeuka kuwa wanyanyasaji wakubwa kwa waume zao, hasa pale wanapotoa fedha za Vicoba na kujiona kichwa katika familia na kuanza kuwadharau wanaume na hata kuwanyima unyumba.

Celestine alisema hali hiyo imekuwa ikisababisha wanaume kufariki dunia kwa mshituko wa moyo na msongo wa mawazo kwa sababu ya kuhifadhi mambo hayo moyoni.

Katika hatua nyingine, wanawake mjini Shinyanga wameiomba serikali kutokomeza matukio ya mauaji dhidi yao kwa kukatwa mapanga na kunyofolewa viungo vyao vya siri.

Katibu wa Jumuiya ya Kikristo Tanzania (CCT) Manispaa ya Shinyanga, Tekla Mongela, alisema hayo jana wakati akisoma risala kwenye maombi hayo ambayo mgeni rasmi alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko.

Alisema changamoto kubwa ambayo inawakabili wanawake ni kuwapo matukio ya mauaji ya wanawake na kunyofolewa viungo vyao vya siri, hali ambayo imekuwa ikiwakosesha amani, hivyo kuiomba serikali ikomeshe matukio hayo.

"Tunaiomba serikali itokomeze matukio ya mauaji dhidi ya wanawake pamoja na kutolewa viungo vyetu ili tuishi kwa amani katika nchi yetu kwa sababu mauaji haya yanatunyima amani," alisema Mongela.

Kwa upande wake, Mboneko alisema serikali itaendelea kuimarisha ulinzi ndani ya jamii pamoja na kuwachukulia hatua waganga wa kienyeji wanaopiga ramli chonganishi na kusababisha mauaji ya watu wasio na hatia.

Mboneko pia aliwataka wanawake wajitokeze kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali za uongozi kwenye uchaguzi mkuu, unaotarajiwa kufanyika Oktoba, mwaka huu.



Rais Dk. John Pombe Magufuli, akimuapisha Gerald Musabila Kusaya, kuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, katika hafla iliyofanyika Ikulu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**

# TV ya mtandaoni yawaponza

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Kisutu imewahukumu watu wawili kulipa faini ya Sh. milioni 10 au kwenda jela kutumikia kifungo cha mwaka mmoja baada ya kupatikana na hatia ya kutuma maudhui kwenye mtandao bila leseni ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano (TCRA).

Washtakiwa hao ni Emmanuel Sisala (32) na mfanyabiashara Juhudi Motda (39) na hukumu dhidi yao ilisomwa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi Augustina Mmbando.

Wakili wa Serikali, Adolf Lema, alidai kuwa kati ya Januari 2018 na Februari 2020, katika Jiji la Dar es Salaam, kupitia televisheni mtandaoni ijulikanayo Jumo Television, walituma maudhui bila leseni ya TCRA.

Washtakiwa walikiri makosa yao na Upande wa Jamhuri uliomba mahakama kutaifisha mitambo na mali mbalimbali ikiwamo simu za mkononi, kamera na kompyuta.

Hakimu Mmbando alisema kwa kuwa washtakiwa wamekiri makosa yao, mahakama yake inawatia hatiani.

Alisema washtakiwa watalipa faini ya Sh. milioni tano kila mmoja na wakishindwa, watakwenda jela kutumikia kifungo cha mwaka mmoja.

"Mahakama hii inaamuru kutaifishwa vielelezo walivyokutwa navyo zikiwamo simu za mkononi kompyuta na kamera," alisema.

Washtakiwa hao walifanikiwa kulipa faini na kuachwa huru na mahakama.

# Wataalamu kutua Zenji mabadiliko tabianchi

**Na Mwandishi Wetu, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Zungu, amaeahidi kupeleka wataalamu wa mazingira ili kufanya tathmini katika eneo la Kwamgogo kisiwani Pemba ambalo limeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi.

Aliyasema hayo kisiwani Pemba jana alipotembelea eneo hilo kujionea athari za kimazingira zilizosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.

Alisema ni lazima jitihada za haraka zichukuliwe katika eneo hilo ili kuepusha Kisiwa cha Pemba kuharibiwa na mabadiliko ya tabianchi.

"Tutaleta watu wafanye tutathmini ni kitu gani tufanye ili kuzuia haya maji kuja tena au kuyazuia yarudi huko yalikotoka na kunusuru eneo hili," alisema.

Kijiji cha Kwamgogo kimeathiriwa na mabadiliko ya tabianchi yaliyosababisha maji kujaa na kuharibu mazingira na wananchi kukosa njia ya kupita wakati wanaenda sokoni au kwenye shughuli zao za kila siku, baadhi wakilazimika kuogelea kwenda ng'ambo ya pili.

**"Namshukuru sana Mkuu wa Mkoa pamoja na wananchi wa eneo hili kwa jitihada mlizofanya kulinda mazingira katika eneo hili," alipongeza.**

Aliwashukuru wananchi wa kisiwa hicho na uongozi wa mkoa kwa kuchukua hatua kwa kupanda mikoko ili kupunguza athari hizo za kimazingira katika kijiji hicho.

"Namshukuru sana Mkuu wa Mkoa pamoja na wananchi wa eneo hili kwa jitihada mlizofanya kulinda mazingira katika eneo hili," alipongeza.

Ziara hiyo ya Zungu kisiwani humo imetokana na maagizo aliyopewa na Makamu wa Pili wa Rais, Balozi Seif Ali Iddi, baada ya kumtembelea ofisini kwake kujitambulisha baada ya kuchaguliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira).

**JAGA AUCTION MART LIMITED.**

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA WA JAGA AUCTION MART LTD**

Kwa idhini tuliyopewa na **MAPAMBAZUKO SACCOSS** tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia tarehe ya tangazo hili kwa wadaiwa wanaotajwa hapo chini walipe deni wanalodaiwa na **MAPAMBAZUKO SACCOSS** pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa MNADA WA HADHARA. Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonyesha hapo chini.

| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 1. | SWEETBERT/MASHINE, ROBERT | NYUMBA | KIMARA-STOP OVER | 19/03/2020 |
| 2. | ELIZABETH/JONATHAN,MWAMWEJO | NYUMBA | MGENI NANI | 13/03/2020 |
| 3. | JOHN, MUKIRYA | NYUMBA | MJI MPYA | 26/03/2020 |
| 4. | ALLY/MUSHI, NDENDE | SHAMBA | KISARAWE | 21/03/2020 |

**MASHART YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazo ambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**JAGA AUCTION MART LIMITED.**
**TABATA BIMA, P.O.BOX 111333, Dar es salaam. Tanzania**
**Tel: 0713-123-427 / 0714-110-026**
**Email: jagauction16@gmail.com**

115658202

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## *Simba, Yanga zinatakiwa kucheza kwa nidhamu*

**WATANI** wa jadi nchini, Simba na Yanga, wanatarajia kukutana katika mechi ya mzunguko wa pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

Mechi hiyo ya watani imekuwa ikihusisha idadi kubwa ya mashabiki na hiyo inatokana na klabu hizo mbili kuwa na wafuasi wengi zaidi ikilinganishwa na timu nyingine zinazoshiriki katika ligi hiyo.

Mara ya mwisho timu hizo zilikutana Januari 4, mwaka huu katika mchezo wa kwanza na matokeo yalikuwa ni sare ya mabao 2-2, Simba ikitangulia kufunga katika kipindi cha kwanza na Yanga ikisawazisha magoli hayo ndani ya dakika nne baada ya kurejea kwenye dakika 45 za mwisho.

Mbali na timu inayoshinda kupata pointi tatu muhimu, Simba ambao ni mabingwa watetezi watashuka uwanjani kuhitaji ushindi ili kujiimarisha kileleni katika msimamo wa ligi hiyo wakati Yanga wanahitaji kuendelea kuwapo katika mbio za kuwania taji hilo.

Mechi hiyo inatarajiwa kutoa picha ya mbio hizo za ubingwa, kwa maana endapo Simba itaibuka na ushindi, itawaacha Azam FC na Yanga mbali wakati Yanga nao wanahitaji ushindi ili kupunguza idadi ya tofauti ya pointi zilizopo sasa, licha ya kucheza michezo miwili pungufu.

Ili mechi hiyo ambayo kwa mara ya kwanza inahudhuriwa na Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Ahmad Ahmad, iwe na mvuto, wachezaji wa timu zote mbili wanatakiwa kuonyesha nidhamu na kuheshimu kanuni 17 za mchezo huo.

Nipashe inawakumbusha wachezaji wa Simba na Yanga kuonyesha wamekomaa na ni wazoefu wa mechi kubwa mbele ya kiongozi huyo wa juu wa mpira Afrika kwa kucheza katika kiwango cha juu na ikiwezekana kumshangaza Ahmad kama nyota hao wanacheza hapa Tanzania.

Si tu kuipa heshima mechi hiyo ya 'dabi', pia itawasaidia kuwatangaza wachezaji husika, kwa sababu ujio huo wa Ahmad utawafanya pia mawakala wa wachezaji nao kuvutiwa kuufuatilia mchezo huo utakaochezeshwa na waamuzi sita.

Refa Martin Saanya kutoka mkoani Morogoro ndiye atasimama katikati katika mechi hiyo na ili mchezo huo kuwa na mvuto, anatakiwa kuongeza umakini na kuchezesha kwa haki mechi hiyo. Endapo mechi hiyo itachezeshwa kwa haki, tunaamini hakuna vurugu au malalamiko yoyote ambayo yatatokea baada ya mchezo huo kumalizika.

Haitapendeza kuona waamuzi wetu wanachezesha chini ya kiwango na kupelekea siku chache baadaye kufungiwa.

Kwa waamuzi wetu kufanya vizuri katika mechi hiyo, kunaweza kuwapa nafasi ya kuteuliwa kuchezesha mechi mbalimbali za kimataifa, kwa sababu katika ugeni wa Ahmad, ameambatana na Mwenyekiti wa Kamati ya Waamuzi ya CAF.

Mara kadhaa, vurugu za wachezaji na mashabiki huanza baada ya kutoridhishwa na uamuzi wa marefa hao ambayo wamepewa dhamana na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).


Na umakini huu wa waamuzi hautakiwi kuwapo katika mechi za Simba na Yanga, umakini huo unatakiwa kuonekana katika mechi zote za Ligi Kuu, hakuna timu ndogo wala timu kubwa, jambo hili la kupendelea baadhi ya timu huleta unyonge hasa kwa klabu ndogo ambazo kikanuni zina haki sawa na vigogo hao wa soka nchini.

Mashabiki pia watakaohudhuria uwanjani katika mchezo huo wanakumbushwa kuwa na nidhamu na watulivu na kamwe kutoingia na matokeo yao.

Ili kuepusha msongamano ni vema mashabiki wakakata tiketi zao mapema na vile vile kufika uwanjani hapo mapema badala ya kusubiri muda wa jioni kuingia watu wengi kwa wakati mmoja na kupelekea msongamano.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Mneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Ukistaajabu ya chawa ...

Na Barnabas Maro

"UKISTAAJABU ya chawa huona ya kunguni." Maana yake ukishangaa kutokana na usumbufu wa chawa utashuhudia makubwa ya kunguni.

Methali hii humfunza mtu anayeshangaa au anayetishwa na mambo madogo kuliko makubwa yanayoweza kutokea au yatakayotokea.

'Upendeleo' au 'upendeleaji' ni tabia ya kufanya jambo kwa kumili (kitendo cha kitu au mtu kuelemea upande mmoja kimawazo au kimatendo) upande fulani; hali, tabia au tendo la kupendelea.

Ligi Kuu ya Tanzania Bara yenye timu 20, kila moja inagombea kutwaa ubingwa, hasa Simba inayotetea ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo, Yanga ambayo ndio bingwa wa kihistoria, Mtibwa Sugar, na Azam.

Hata hivyo yashangaza kusikia timu ya Yanga 'ilisahauliwa' kupangwa kwenye mechi za viporo za mzunguko wa kwanza.

Haiingii akilini kuambiwa eti 'viporo' vya Yanga vilisahauliwa kupangwa. Je, wahusika walikuwa wamelewa au walikuwa na lao jambo? Eti bila soni, wakaomba msamaha kwa tendo hilo!

Nikiulizwa kama Shirikisho la Soka nchini (TFF) linafanya kazi yake ipasavyo, jibu langu ni HAPANA kwa herufi kubwa. Huwaje Shirikisho hilo lizinduke baada ya watazamaji kulalamikia uamuzi wa marefa?

Viongozi hao hawaoni mauzauza (hali ya macho kudanganyika na kuyafanya yaone kitu ambacho sivyo kilivyo; hali ya kutoeleweka; shaghalabaghala)?

Kama watazamaji wanaona kila kinachotokea, viongozi huwa wanasinzia (patwa na usingizi wa ghafla na kwa muda mfupi, kuwa na dalili za kutaka kulala kwa kufumbafumba macho) uwanjani? Kama ndivyo, huenda kufanya nini?

Runinga ya Azam ina picha za michezo yote ya Ligi Kuu. Hivyo viongozi wa TFF wanapaswa kuomba picha za mchezo mzima, wakiwamo waamuzi waliochezesha mechi zinazolalamikiwa.

Pia wawepo washika vibendera wa mechi zinazolalamikiwa, makamisaa na viongozi wa chama cha waamuzi. Kwa pamoja waangalie picha hizo na kulinganisha na kanuni 17 za mchezo wa kandanda kisha watoe uamuzi wa haki kwa pande zote.

Kadhalika timu 'iliyopewa' ushindi inyang'anywe na badala yake ipewe timu iliyodhulumiwa. Hata kama kuna timu 'iliyosawazisha' kwa namna isiyokubalika, ipokonywe alama moja na kupewa timu pinzani.

Waamuzi na wasaidizi wao waadhibiwe na kupewa onyo kuwa endapo watarudia tena wataachishwa kuchezesha mechi yoyote ndani na nje ya nchi na nakala ya uamuzi huo kupelekwa Shirikisho la vyama vya kandanda Afrika na lile la dunia, FIFA.

Kadhalika makamisaa waadhibiwe kama walikuwa kimya bila kufikisha TFF matukio yote yaliyokiuka kanuni za FIFA uwanjani. Kama walinyamaza tu, basi nao walihusika kuharibu mchezo. Adhabu inayowafaa ni kuwaondoa kwenye ukamisaa.

Vilevile ikijulikana kuwa viongozi waliotajwa, na wa vilabu husika kwenye mchezo huo walihusika kutoa au kupokea rushwa, nao wapelekwe kunakohusika - Takukuru kuchunguzwa.

Utaratibu huu utawakomesha wanaokwenda kwa wachawi wanapogombea nafasi za uongozi kwenye vilabu vya kandanda na hata TFF ili wachaguliwe!

Kama taratibu nilizotaja hazitatekelezwa, Wallahi! (kwa jina la Mwenyezi Mungu; tamko la kiapo cha kuthibitisha kuwa lilosemwa ni kweli) basi kandanda la Tanzania litazidi kudorora, huku viongozi wa vilabu na vyama vya kandanda wakiendelea kujinufaisha!

Jambo lingine la kuzingatia ni vilabu kuwanyima baadhi ya wachezaji wao kwenda kujiendeleza nchi za nje, hasa Ulaya kwenye maendeleo na malipo mazuri kuliko kwetu.

Kadiri watakavyoruhusiwa kwenda nje ya nchi ndivyo watakavyozidi kujiendeleza kimpira na kuiletea nchi faida: Kupata wachezaji wazuri watakaounda timu za taifa, kuinufaisha nchi na vilabu vyao vya zamani kwa kuingiza fedha za kigeni nchini. Enyi viongozi wa vilabu vya kandanda sikieni:

"Akubalie kurudiwa huwa katika njia ya uzima, bali yeye aachaye maonyo hukosa. Yeye afichaye chuki ana midomo ya uongo, na yeye asingiziaye ni mpumbavu. Katika wingi wa maneno hapakosi kuwa na maovu, bali yeye azuiaye midomo yake hufanya akili." (Mithali 10:17-19).

Mwisho nawausia (kataza jambo fulani kwa maneno yenye hekima; kitendo cha kutoa maelekezo ya hekima kwa mtu) wachezaji kununua au kununuliwa magari. Kwa nini hawaombi kujengewa nyumba za kuishi badala ya magari yasiyokuwa na faida kwao? Wanapaswa kutafakari.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

## HABARI PICHANI

# ZIARA YA KATIBU MKUU WA CCM DK. BASHIRU ALLY KATIKA VYOMBO VYA HABARI VYA IPP



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally (kushoto), akisalimiana na baadhi ya wahariri na viongozi wa kampuni ya The Guardian Ltd (TGL), inayochapisha magazeti ya The Guardian an Nipashe, baada ya kuwasili katika ofisi za kampuni hiyo, katika eneo la Viwandani, Mikocheni, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA ZOTE: JOHN BADI**



Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Dk. Bashiru Ally (wa pili kulia), akitembelea kiwanda cha kuchapisha magazeti cha TGL. Kulia ni Mkurugenzi wa IPP Ltd, Joyce Luhanga, Meneja wa Rasilimali watu na Mwanasheria wa TGL, Emmanuel Matondo (wa pili kushoto) na Kaimu Meneja Rasilimali watu Mwandamizi, Ayoub Semvua.



Dk. Bashiru, akifanya mahojiano katika studio za East Africa Redio.



Dk. Bashiru, akipata maelezo kutoka kwa Mkuu wa Idara ya Habari wa ITV, Stephen Chuwa.



Dk. Bashiru, akiwa katika studio ya Redio One. Kushoto ni Mkurugenzi wa Radio One, Deogratius Rweyunga na (wa tatu kushoto), ni Mkurugenzi Mtendaji wa ITV na Redio One, Joyce Mhavile.



Dk. Bashiru, akipata maelezo kutoka Mkurugenzi wa Chaneli ya ITV na Capital TV, Macharia Koigi, alipotembelea studio ya ITV.

# Madaktari, manesi walalamikiwa kutolea lugha chafu wajawazito

**Na Shaban Njia, MBOGWE**

WAJAWAZITO wilayani Mbogwe mkoani Geita, wamewalalamikia wauguzi na madaktari wa Hospitali ya Halmashauri hiyo kuwatolea lugha chafu wakati wanapokwenda hospitalini hapo kujifungua na kwamba hatua hiyo imesababisha wengi wao kujifungulia nyumbani.

Malalamiko hayo yalitolewa jana wakati Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, Martha Mkupasi, akisoma taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, mwaka jana.

Angelina Mathias, mkazi wa Kata ya Nyakafulu, alisema lugha chafu zinazotolewa na wauguzi na baadhi ya madaktari wa hospitali ya wilaya ndicho chanzo cha wajawazito kujifungua nyumbani licha ya kujua ni hatari kwa maisha ya mama na mtoto.

"Mkuu wa Wilaya, hatupendi kuendelea kujifungulia majumbani (nyumbani) mwetu (kwetu) ila inatulazimu baada ya kuwa tunatolewa maneno machafu na baadhi ya wauguzi hasa wakati wa kusukuma mtoto," alisema.

"Sisi wajawazito kuna baadhi ya dawa huwa tunatakiwa kuzitumia kipindi cha ujauzito, zinapokosekana hospitalini hutulazimu kwenda kununua kwenye maduka ya nje, tunapohoji juu ya ukosefu wa dawa hizo wanatwambia tukamhoji Rais (John) Magufuli," aliongeza.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dk. Kunye Clint, alikiri kuwapo kwa malalamiko hayo hospitalini na kusema kuwa hayo yote yanajitokea kutokana na baadhi ya wauguzi na madaktari kutokuwa na maadili ya utumishi wa umma.

Pia alisema hivi karibuni atafanya vikao na waguzi na madaktari wote ili kuwakumbusha wajibu wao wa kazi na kutojiingiza katika vitendo vya kuomba na kupokea rushwa ambavyo ni kinyume cha taratibu za kazi.

Naye Katibu wa CCM Wilaya ya Mbogwe, Grace Shindika, alisema wakati wanatafuta rufani ya kumpeleka Muhimbili aliyekuwa mwenyekiti wa chama hicho, alirushiwa maneno machafu na mmoja wa wauguzi na kusababisha rufani kuchelewa kutoka.

Katika hatua nyingine, Mkupasi alisema kumeibuka tabia kwa baadhi ya wazazi wenye watoto waliopewa ujauzito wakiwa masomoni kukutana na kumalizana na kumwacha mtoto akihangaika na ujauzito.

Alisema katika Kituo cha Polisi Mbogwe, kuna kesi nyingi za wanafunzi kupewa ujauzito lakini hazina ushahidi wa kuwatia hatiani waliohusika baada ya wazazi wa pande mbili kukutana na kumalizana.

# Ataka wanawake kuchangamkia fursa

**Na Mwandishi Wetu, BARIADI**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, amezindua maonyesho ya wajasiriamali na huduma na kuwataka wakazi wa Simiyu, hasa wanawake, kujitokeza kuchangamkia fursa ili kujikwamua kiuchumi.

Aliyasema hayo jana katika hafla hiyo ambayo iliambatana na mapokezi ya msafara wa kijinsia uliokuwa ukizunguka katika mikoa tisa kutoa elimu ya kupambana na vitendo vya ukatili wa kijinsia.

Maonyesho hayo ni sehemu ya kuelekea kilele cha maadhimisho ya kitaifa ya Siku ya Wanawake Duniani yatakayohitimishwa kesho mjini hapa.

Waziri Ummy aliwapongeza Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka na Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto anayeshughulikia Maendeleo ya Jamii, Dk. John Jingu, kwa kufanikisha maadhimisho hayo.

Kuhusu uboreshaji wa bidhaa lishe, alisema Wizara ya Kilimo na Wizara ya Afya, zinaweza kushirikiana kuboresha chakula lishe kwa watoto na kukabiliana na udumavu kwa watoto.

"Tukishirikiana kuwawezesha wanawake hawa kutumia teknolojia rahisi kukabiliana na udumavu kwa watoto," alisema.

Pia alipongeza huduma na elimu kupitia misafara ya kupinga ukatili wa kijinsia iliyoratibiwa na wizara yake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali.

"Misafara hii imewafikia watu wengi, hivyo kupata elimu itakayowasaidia kuondokana na vitendo vya ukatili," alisema.

Mwalimu aliongeza kuwa anazo taarifa za wanaume wanaopata vipigo kutoka kwa wenza wao, hivyo wasione aibu kutoa taarifa kwenye madawati ya jinsia kwa ajili ya kupata msaada.

"Ingawa unyanyasaji wa vipigo uko kwa wanawake, wanaume msiogope kuripoti pale mnaponyanyaswa ili mpate msaada," alisema. Naye Dk. Jingu alisema wizara kwa kushirikiana na wadau, imejizatiti kuhakikisha inatoa elimu kwa jamii ili kuondokana na vitendo vya ukatili wa kijinsia

Alisema kupitia makongamano na msafara wa kijinsia, Wizara imewafikia wadau wengi na lengo lilikuwa ni kuwafikia Watanzania katika ngazi mbalimbali.

Akitoa salamu za Wizara ya Kilimo, Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hussein Bashe, alisema wizara yake inatambua mchango wa wanawake katika sekta hiyo.

"Kila penye wakulima wanne, watatu ni wanawake hivyo mchango wa wanawake katika kilimo ni mkubwa sana tunautambua sana mchango wenu wanawake" alisema

Maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani kwa mwaka huu, yanaongozwa na kaulimbiu ya isemayo "Kizazi cha Usawa kwa Maendeleo ya Tanzania ya Sasa na Baadaye".



Mkuu wa Mkoa wa Katavi, Juma Homera, akisalimiana na mmoja wa watumishi ofisini kwake, jana, kwa kutumia miguu, ikiwa ni utekelezaji wa ushauri wa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, dhidi ya kujihami na maambukizi ya ugonjwa wa corona. **PICHA: DAR24 MEDIA**

# Uchunguzi huduma bwawa wakamilika

**Na Godfrey Mushi, SAME**

MKUU wa Wilaya ya Same mkoani Kilimanjaro, Rosemary Senyamule, amesema uchunguzi dhidi ya watu wanaodaiwa kuhujumu mradi wa bwawa la umwagiliaji la Kalimawe lililoko wilayani hapa, umekamilika.

Wanaochunguzwa kuhusiana na sakata hilo ni pamoja na viongozi wa serikali ngazi ya kijiji. Watu hao wanadaiwa kuing'oa mitambo hiyo na kuiondoa eneo hilo.

Jana, Senyamule alithibitisha kuwa uchunguzi dhidi ya watu wanaotuhumiwa kuhujumu mradi huo umekamilika.

Alisema tayari vyombo vya dola vimekamilisha kazi hiyo, baada ya viongozi hao kupewa nafasi ya kutubu hadharani na kisha kuirejesha mitambo ya kufua umeme wa jua iliyochukuliwa kiutata.

Watu wanaodaiwa kuwa viongozi wa umma wakishirikiana na baadhi ya wananchi katika Kijiji cha Karamba, Kata ya Kalimawe, waling'oa mitambo hiyo iliyokuwa ikitumika kusukuma maji.

Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya aliwataka wakazi wa Karamba kuheshimu na kuendelea kushirikiana na vijiji vingine vinavyolizunguka Bwawa la Kalimawe vinavyotekeleza mradi wa kuzalisha vifaranga vya samaki.

Mwaka jana, vijiji vinne viliingia makubaliano ya ubia katika uwekezaji huo na Kampuni ya Norway na ile ya Mikono Tayari ya Tanzania.

Kampuni hizo zimeahidi kujenga kiwanda cha kisasa cha kusindika minofu ya samaki kwa ajili ya soko la ndani na la kimataifa.

Bwawa hilo lenye urefu wa mita 4,000 na upana wa mita 5,000 lilijengwa na serikali ya wakoloni, kati ya mwaka 1952 na 1959.

**Alisema tayari vyombo vya dola vimekamilisha kazi hiyo, baada ya viongozi hao kupewa nafasi ya kutubu hadharani na kisha kuirejesha mitambo ya kufua umeme wa jua iliyochukuliwa kiutata.**

# BoT yaanzisha dawati malalamiko kwa wateja

**Na Allan Isack,ARUSHA**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema imeanzisha dawati la malalamiko na mpaka sasa imepokea malalamiko 496 kutoka kwa wateja kuhusu huduma mbalimbali za kibenki.

Akizungumza juzi jijini hapa wakati wa semina ya waandishi wa habari za uchumi na biashara, Meneja Msaidizi wa Dawati la Malamiko kutoka BoT, Ganga Mlipano, alisema kitengo hicho kimepokea malalamiko 496 na kati ya hayo, 40 yametatuliwa.

Alitaja malalamiko hayo kuwa mikopo au mikataba migumu, kutumia lugha mbaya kwa wateja, kutumia lugha ya kiingereza, kuchelewesha kurudisha au kutorudishiwa hati ya nyumba au kadi za magari na kukataliwa kuhama benki moja kwenda nyingine.

Alisema kati ya malalamiko hayo, asilimia 90 ya walalamikaji wanatoka katika Mkoa wa Dar es salaam.

Hata hivyo, alisema malalamiko yanatatuliwa kwa mujibu wa Miongozo ya Benki Kuu Kuhusu Malalamiko ya Wateja wa Benki ya Mwaka 2015 ambayo inaeleza namna ya kupokea na kuyatatua malalamiko.

Mlipanio pia alisema dawati linatatua malalamiko hayo kwa kufuata misingi ya kimataifa bila kuwa na gharama yoyote, upendeleo, uhuru na uwazi.

"Mlalamikaji anapaswa kwanza kupeleka malalamiko yake kwenye benki yake na benki hiyo inapaswa kutatua malalamiko hayo ndani ya siku 21 na asiporidhika au benki hiyo ikikaa kimya, ndipo anapaswa kuleta malalamiko kwenye dawati letu," alisema.

Pia alisema dawati hilo limetatua malalamiko mengi na wananchi wamepata chombo cha uhakika cha kuwasilisha malalamiko yao.

Sambamba na hilo, alisema wananchi wanakabiliwa na uelewa mdogo kuhusu dawati hilo na idadi ndogo ya malalamiko kutoka kwa wananchi wa mikoani.



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru, Emmanuel Mkongo, akizungumza wakati wa ufunguzi wa mafunzo ya mfumo wa kutunza taarifa za wanafunzi wa Shule za msingi (PReM), kwa wakuu wa shule za sekondari za serikali na binafsi, yaliyofanyika, wilayani humo, mkoani Arusha juzi. Kushoto ni Ofisa Elimu ya Sekondari wa Halmashauri hiyo, Emmy Mfuru. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Serikali yafurahia ujenzi na ukarabati shule mradi EP4R

**Na Allan Isack, ARUMERU**

SERIKALI kupitia miradi ya lipa kutokana na matokeo 'Education Payment for Result' (EP4R), imejenga na kuboresha miundombika kwenye shule mbalimbali za msingi na sekondari katika halmashauri ya Arusha DC, Arumeru mkoani hapa, ili kuboresha miundombinu ya shule.

Akitoa taarifa kwa vyombo vya habari, Ofisa Habari wa Halmshauri ya Arusha DC, Elinipa Lupembe, alisema kwa kipindi cha miaka minne serikali imejenga na kuboresha miundombinu ya shule za msingi na sekondari.

Lupembe alisema katika Shule ya Sekondari ya Mlangarini, serikali imejenga madarasa mapya, mabweni ya wanafunzi wa kike na wa kiume, maabara ya masomo ya sayansi na kukarabati baadhi ya madarasa.

Licha ya hayo, alisema serikali imeipandisha hadhi shule hiyo kuwa ni miongoni mwa shule za mchepuo wa kidato cha tano na cha sita wilayani humo.

Pia alisema serikali imekuwa ikitoa mamilioni ya fedha kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule hiyo ili iwe na hadhi ya shule za kidato cha tano na sita. Mwaka wa fedha wa 2016/17, alisema serikali ilitoa Sh. milioni 250 ambazo zilijenga bweni lenye uwezo wa kuchukua wasichana 80, ujenzi wa vyumba sita vya madarasa, ukarabati wa maabara tatu za masomo ya sayansi na ujenzi wa vyoo vya wanafunzi.

Alisema kutokana na kufanya vizuri shule hiyo katika matokeo ya kidato cha pili na cha nne, mwaka wa fedha 2018/19, serikali ilitoa Sh. milioni 110 kwa ajili ya ujenzi wa maktaba na ukarabati wa bwalo la chakula na ujenzi huo umekamilika.

Lupembe alisema mkakati wa serikali ni kupandisha kiwango cha taaluma shuleni hapo kwa kuweka mazingira bora ya kujifunzia kwa wanafunzi na ya kufundishia kwa walimu ili kuleta matokeo chanya wa shule za msingi na sekondari.

Uongozi wa Halmashauri ya Arusha DC, umewataka wananchi na wadau wa elimu kuunga mkono juhudi za serikali kuchangia ujenzi na uboreshaji wa miundombinu ya shule za serikali, ili wanafunzi wapate elimu katika mazingira bora na rafiki.

## Sirro afungua kituo Yaeda

**Na Allan Isack,MBULU**

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Inspekta Jenerali (IGP), Simon Sirro, amefungua Kituo cha Polisi Bonde la Yaeda Chini wilayani Mbulu mkoani Manyara.

Kufunguliwa kwa kituo hicho, kutapunguza na kukomesha matukio ya mauaji, wizi wa mifugo na unyanyasaji wa kijinsia uliokithiri katika eneo hilo.

Akizungumza juzi wakati wa uzinduzi wa kituo hicho, Sirro alisema ametoa gari moja na kuchangia Sh. milioni 10 kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za askari polisi.

Mkuu huyo wa polisi alimpongeza Mkuu wa Wilaya ya Mbulu, Chelestino Mofuga, kwa usimamzi wa ujenzi wa kituo hicho kilichogharimu Sh. milioni 80.

Alisema Mofuga ameonyesha nia ya kuwajali wananchi wa eneo hilo kwa kufanikisha ujenzi wa kituo cha polisi na kwamba kituo hicho kitasaidia shughuli za ulinzi wa raia na mali zao kwenye eneo hilo.

"Nawapongeza sana kwa hatua hii. Nami nawaahidi baada ya wiki moja nitawaletea gari litawasaidia askari kufanya shughuli za ulinzi wa mali za raia wa eneo hili," alisema IGP Sirro.

Kwa upande wake, Mofuga alisema alibuni wazo la kujenga kituo hicho baada ya kuongezeka matukio ya mauaji ya watu, wizi wa mifugo na unyanyasaji wa kijinsia.

Alisema katika utumishi wake, eneo hilo lilitaka kumwingiza majaribuni kwa kushamiri kwa matukio hayo lakini alishirikiana na wadau kujenga kituo hicho cha polisi.

"Baada ya kuona matatizo yanaongezeka niliunda kamati ya kufanya uchunguzi wa chanzo cha matukio haya ili kukabiliana nayo kwa ajili ya kuleta amani.

"Pamoja na hayo tumefanya harambee ya ghafla na kupatikana Sh.milioni 20 ambazo zimetumika kujenga nyumba za askari polisi," alisema Mofuga.

Mbunge wa Jimbo la Mbulu Vijijini, Flatei Massay, amemshukuru IGP Sirro kwa kuzindua Kituo cha Polisi cha Yaeda Chini huku akisema kitatumika kwa maslahi ya jamii ya eneo hilo.

"Tunaahidi kushirikiana na askari polisi wa eneo hili kwa kuwa wananchi wana mwamko mkubwa kuhusu suala la ulinzi na usalama wa Bonde la Yaeda Chini," alisema Massay.

# 'Ukatili wa kijinsia bado tishio nchini'

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

KANSELA Mkuu wa Ushirikiano na Maendeleo wa Serikali ya Canada kupitia ubalozi wake nchini, Gwen Walmsley, amekutana na wadau kutoka mashirika 39 ya kiraia yanayojishughulisha na masuala ya haki za binadamu kupokea matokeo ya stadi ya awali ya ukatili wa kijinsia katika mikoa ya Kilimanjaro na Arusha.

Walmsley alikwenda mkoani Kilimanjaro jana kuzindua awamu ya pili ya mradi wa kukuza usawa wa kijinsia kwa kutumia elimu ya haki za binadamu.

Mradi huo wa miaka mitano umekuwa ukitekelezwa nchini tangu mwaka 2019 na Shirika la Tusonge CDO kwa ufadhili wa Serikali ya Canada kupitia uhusiano wa kimataifa na wabia wa Taasisi ya Equitas.

Katika Mkoa wa Kilimanjaro, mradi huo unatekeletezwa kwenye Halmashauri ya Manispaa ya Moshi na Wilaya ya Siha, wakati mkoani Arusha, unatekelezwa Jiji la Arusha na Wilaya ya Meru.

Kansela Walmsley alipewa taarifa na Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Tusonge, Agnatha Rutazaa, licha ya jitihada nyingi zilizofanyika kulinda haki za msingi za binadamu, bado hakuna usawa hasa kwa wanawake na wasichana.

"Kwa hali ya sasa, ukatili wa kingono umekithiri kwa wanawake na watoto, wanawake hawaruhusiwi katika kufanya uamuzi wa kipato cha familia na mara nyingi kinamama wanaachwa nyuma katika kufanya uamuzi wa matumizi ya mapato ya familia na wasichana hawapewi fursa ya elimu.

"Kansela Mkuu wa Ushirikiano na Maendeleo katika Ubalozi wa Canada ambao ndiyo wanafadhili mradi huu, amekuja kutuunga mkono na kushirikiana pamoja nasi.

"Lengo kubwa la kufika hapa Moshi ni kufanya uzinduzi wa mradi rasmi na kuangalia kipengele kikubwa cha kurejesha matokeo ya stadi ya awali yaliyofanyika Oktoba mwaka 2019. Stadi hiyo imefanyiwa uchambuzi na matokeo yake yatangazwa Machi mwaka huu," alisema.

Kwa mujibu wa Rutazaa, wadau hao watapata fursa ya kutoa maoni yao kama kuna mawazo au maoni ya mambo ambayo yalionekana yako kwenye jamii, lakini hayakujitokeza wakati wa upimaji na tathmini.

"Tunarejesha matokeo hayo ya stadi ya awali kwa wadau muhimu wa haki za binadamu katika Mkoa wa Kilimanjaro na mradi utatumia mbinu shirikishi katika kukuza usawa wa kijinsia ikijumuisha kujenga uelewa na uwezo, kushirikiana katika kampeni za uhamasishaji, mipango tekelezi ya jamii na majukwaa," alisema.

Lengo la baadaye la mradi huo ni kuwapo kwa ongezeko la uwezo wa wanawake na watoto wa kike katika kukuza usawa wa kijinsia ndani ya jamii.



Mmoja wa wawezeshaji wa mradi wa kukuza usawa kwa kutumia elimu ya haki za binadamu, unaotekelezwa na Shirika la Tusonge kwa ufadhili wa taasisi ya kimataifa ya Equitas, Daudi Massawe, akitoa mrejesho kuhusu stadi ya awali ya ukatili wa kijinsia, katika mkutano wa wadau wa mashirika ya kiraia kutoka mikoa ya Arusha na Kilimanjaro, uliofanyika katika Manispaa ya Moshi, jana. **PICHA: GODFREY MUSHI**

# Wataka bibi mjane asaidiwe kunusuru mali za mumewe

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

UONGOZI wa Kijiji cha Manushi Ndoo, Kata ya Kibosho Magharibi wilayani Moshi, umepeleka kilio kwa wanaharakati wa haki za binadamu, ukitaka waingilie kati sakata la mjane, Aisha Hatibu (76), kukamatwa na kutaka kupokwa ardhi na ndugu wa mume wake.

Aisha mwenye watoto wanane, amedai mgogoro huo umeigawa familia yake kutokana na manyanyaso wanayopata kutoka kwa ndugu wa mumewe.

Ombi la kutaka wanaharakati kujitokeza kumsaidia mjane huyo kumiliki ardhi yenye ukubwa wa ekari 4.5, lilitolewa jana na Ofisa Mtendaji wa Kata ya Kibosho Magharibi (WEO), Elisha Moses, wakati wa mkutano wa wanaharakati wanawake walioitishwa na Jukwaa la Vuguvugu la Ukombozi wa Mwanamke Kimapinduzi (Tapo).

"Leo mmekuja kwetu kutupa elimu kuhusu masuala mbalimbali kama migogoro ya ardhi, mirathi, ukatili wa kijinsia, ndoa na haki ya kurithi mali kwa wanawake.

"Niwaombe wanaharakati wote mliokuja kutupa elimu, msaidieni na mjane Aisha ambaye amepata ugonjwa wa shinikizo la damu kutokana na mgogoro wa ardhi kati yake na familia ya marehemu mumewe," aliomba.

Awali akizungumzia tukio hilo, Aisha alisema tangu mumewe afariki dunia mwaka jana, amekuwa katika mgogoro mkubwa na familia hiyo ya mumewe kutokana na ndugu wa kiume wa mumewe kutaka kurithi shamba hilo, wakidai mke wa marehemu hana haki kimila kulimiliki.

Mtoto wa kiume wa mjane huyo, Yusuph Hatibu, akizungumza katika mkutano huo, alisema tangu mgogoro huo ulipochomoza, mama yake ni mgonjwa na amekuwa akipambana kuhakikisha analinda haki yake.

Ofisa wa Haki za Binadamu wa Shirika la Kwieco, Elizabeth Mushi, alisema wasaidizi wa kisheria na wanaharakati wamepokea suala hilo na watamsaidia mjane huyo kumiliki haki yake kimila au kisheria.

"Siku hizi kuna hati za kimila ambazo zinatambulika kisheria na kuna hati za kisheria ambazo hutolewa na serikali, tutatafuta haki yake hata mahakamani. Mama usijali ndiyo maana tumekuja Manushi Ndoo kuwapigania, maana tunajua mila zinakandamiza wanawake,"alisema.

Ofisa huyo alisema tatizo kubwa linalokwamisha juhudi za wadau kutokomeza ukatili wa kijinsia katika eneo hilo, ni wazazi kumalizana kienyeji na watuhumiwa.

# Kigogo CCM asaka tiba mimba kwa wanafunzi

**Na Mwandishi Wetu, SIHA**

KATIBU wa Jumuiya ya Wazazi ya Chama cha Mapinduzi (CCM), Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro, Omary Kisesa, ameitisha kikao maalum cha baraza hilo kujadili namna ya kupata mwarobaini wa mimba kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari wilayani humo.

Jana, wakati akizungumza na wajumbe wa baraza hilo, kigogo huyo alisema jumuiya hiyo ambayo ina jukumu la kusimamia malezi na maadili, ina kila sababu ya kupinga ukatili huo unaoendelea kuvuruga taswira ya kundi hilo katika kupata elimu.

"Wazazi na walezi wanatakiwa kuwa mstari wa mbele kuwalinda watoto wa kike na kuhakikisha hawakatishwi masomo kwa kupewa mimba wakiwa katika umri mdogo, hasa kipindi cha likizo wanapokuwa majumbani," alisema.

Kisesa alisema jumuiya hiyo haipendezwi na takwimu za wanafunzi waliokatishwa masomo kwa miaka miwili mfululizo wilayani humo na kwamba sasa watawatumia watu mbalimbali kulikabili tatizo hilo.

Alibainisha kuwa takwimu za walioacha shule kutokana na ujauzito mwaka 2019 zinaonyesha kwa ni vijana 24 na mwaka huu tayari wanafunzi sita wameshakumbwa na baa hilo.

"Hapa leo tumejadili mambo mbalimbali ya maendeleo, lakini pia mmeona kuanzia Januari mwaka huu mpaka Machi kumeripotiwa mimba sita, hata mwaka haujaisha.

"Kuna taarifa kwamba wanafunzi hao walipata mimba wakiwa likizo, sasa kama baraza lazima tuweke mikakati ya kumaliza jambo hili,"alisema.

Mmoja wa wajumbe wa baraza hilo, Michael Mollel, ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo Kata ya Donyomoruwaki, alisema kwa sasa wamepanga kupunguza mimba za utotoni kwa kupiga marufuku watoto wa kike kushiriki ngoma za jamii ya wafugaji wa Kimasai.

**"Hapa leo tumejadili mambo mbalimbali ya maendeleo, lakini pia mmeona kuanzia Januari mwaka huu mpaka Machi kumeripotiwa mimba sita, hata mwaka haujaisha.**

# UWT yaomba nafasi zaidi za uongozi

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

KATIBU Mkuu wa Umoja wa Wanawake wa Tanzania (UWT), Queen Mlozi, amemwomba Rais John Magufuli kuendelea kutoa nafasi za uongozi kwa wanawake ili kufikia usawa wa kijinsia wa 50 kwa 50.

Mlozi alitoa ombi hilo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari katika kuelekea Siku ya Wanawake Duniani inayofanyika Machi 8, kila mwaka. Kwa mwaka huu, maadhimisho ya siku hiyo kitaifa yatafanyika mkoani Simiyu.

Alisema wanawake waliopewa nafasi za uongozi katika serikali ya awamu ya tano wameonekana kufanya vizuri kwenye utendaji wao, hivyo kumwomba Rais kuendelea kuwaamini na kuwapa nafasi zaidi.

"Serikali imeweka historia ya pekee kwa kuteuliwa kwa Makamu wa Rais mwanamke, Samia Suluhu Hassan, Naibu Spika mwanamke, Dk.Tulia Ackson, Mawaziri, Manaibu na ngazi nyingine mbalimbali. Tunaomba Rais wetu aendelee kutoa nafasi zaidi kwa wanawake," alisisitiza.

Alibainisha kuwa kuaminiwa kwa wanawake kutaifanya Tanzania kufikia 50 kwa 50 kwenye nafasi mbalimbali za uongozi, hivyo kuwataka wanawake kujiamini na kuwa waadilifu kwenye utendaji wao ili waendelee kuaminiwa zaidi.

"Acheni unyonge, kinachotakiwa ni usawa kati ya mwanamke na mwanamume," alisema.

Kuhusu uchaguzi mkuu mwaka huu, Mlozi aliwataka Watanzania kuwachagua viongozi ambao wana uwezo wa kutafsiri Ilani ya Uchaguzi ya CCM.

"Sisi wanawake tunajivunia utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwa kuwa iko miradi mingi inayogusa wanawake imetekelezwa kwa mfano huduma za afya ujenzi wa vituo vya afya na miradi ya maji. Hii inafikia azma ya kumtua mama ndoo kichwani," alisema.

Aliwataka wanawake kumpigia kura za kishindo Rais Magufuli na viongozi wengine watakaojitojeza kuchukua fomu kwa ajili ya kugombea nafasi mbalimbali hususani wanawake ili kuendelea kuinua uchumi wa taifa.

"Kwa miaka minne tumeona maajabu makubwa yamefanywa. Naamini akipewa miaka mitano mingine atafanya maajabu makubwa zaidi," alisema.

Mlozi alisema wanwake ni kioo cha jamii na kielelezo, lazima wawe kifua mbele kupambana na udhalimu, ukatili na unyanyasaji wa kijinsia wa aina yeyote.



Mkalimani wa lugha ya alama, Mwalimu Faimes Mwakatobe (kushoto), akiwatafsiria wanafunzi wenye ulemavu wa kutosikia wa Shule ya Sekondari ya Dodoma, wakati wa mkutano wa wadau wa elimu uliofanyika shuleni hapo, jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Daktari bingwa ataja vitu vinavyoathiri masikio

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

DAKTARI Bingwa wa magonjwa ya masikio katika Hospitali ya Benjamini Mkapa, Dk. Faustine Mayalla, ametaja vitu vinavyoathiri usikivu kwenye masikio kuwa ni pamoja na matumizi ya visikilizi (Earphone).

Alisema hayo juzi katika upimaji wa masikio uliofanyika kwenye Shule ya Msingi Nghong'onha jijini hapa.

Dk. Mayalla alisema watu wanatakiwa kuacha matumizi ya 'earphone', kukaa sehemu zenye sauti kubwa kwa kuwa zinachangia kuathiri masikio.

"Pia wanatakiwa kuacha kusafisha masikio kwa kutumia pamba kwa kuwa inasukuma uchafu ndani na kuharibu usikivu," alisisitiza.

Dk. Mayalla alisema usafishaji wa masikio kwa kutumia pamba unazidi kuharibu masikio kwa kuendelea kusukuma uchafu ndani.

"Nitoe wito kwa jamii kuacha hii tabia ya kusafisha masikio kwa kutumia pamba, hapa naomba muache kabisa hii sio njia sahihi ya kusafisha masikio, kwani masikio hujisafisha yenyewe, matumizi ya pamba yanaweza kupelekea kupoteza usikivu kabisa," alisema.

Alitoa rai kwa jamii pindi wanapoona wanapoteza usikivu au masikio kuuma kuwahi hospitalini ili kupata huduma haraka kabla ya kupoteza usikivu.

"Tumesikia hapa kuwa kuna baadhi ya watu wakiona wanapata maumivu ya sikio huweka mafuta ya kuku,au wanasaga nyanya na kuweka hii sio njia sahihi, ukihisi dalili za maumivu wahi hospitali kupata huduma haraka kwani usikivu ndio kila kitu," alisisitiza.

Aidha, aliwataka wafanyakazi wa viwandani kuwa na vidhibiti sauti kwa kuwa kuna kelele na kunasababisha kupoteza usikivu.

Kuhusu kliniki hiyo, daktari huyo alisema wanafunzi 71 walibainika kuwa na shida ya masikio kwenye shule hiyo na baadhi yao wametibiwa papo hapo.

Kwa upande wake, Mwalimu wa Shule hiyo, Ezekiel Lubuva, aliishukuru hospitali hiyo kwa kutoa huduma hiyo kwa kuwa wanafunzi wamekuwa wakipata shida ya usikivu bila kupata huduma.

Mmoja wa wanafunzi waliopatiwa huduma hiyo, Karoline John alisema kwa muda mrefu amekuwa akiteseka kutosikia vizuri lakini kwa sasa amejua tatizo linalomsumbua baada ya kufanyiwa vipimo na kupewa matibabu.

# Kongamano kuboresha elimu laja

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

KUTOKANA na kushuka kwa kiwango cha ufaulu, Mkoa wa Dodoma unatarajia kufanya kongamano la siku mbili kwa wadau wa elimu ili kuangalia chanzo cha tatizo hilo.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa kongamano hilo litafanyika Machi 21 hadi 22, mwaka huu na litafunguliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Alisema hali ya maendeleo ya elimu kwa mkoa huo si ya kuridhisha na viko baadhi ya viashiria vinavyosababisha kushuka kwa kiwango hicho licha ya kuwapo mambo mazuri yanayofanywa na serikali mkoani hapa.

"Mfano watoto wengi hawasomi saa zilizopangwa kwa siku kutokana na wengi kukaa mbali na eneo ilipo shule. Utakuta mtoto anasafiri umbali mrefu na kufika shuleni amechelewa na kuchoka, hivyo kushindwa kufuatilia vipindi darasani," alisema.

Dk. Mahenge pia alisema kuna uhitaji mkubwa wa mabweni ili kusaidia watoto kuwa karibu na shule.

"Hata wanaotoka maeneo jirani na shule ikifika saa nne au saa saba wanakwenda nyumbani kula na si wote wanaorudi darasani. Hapa kuna jambo la kufanya. Bado kunatakiwa usimamizi wa karibu wa ufuatiliaji kwa ngazi zote ili kuhakikisha vipindi vilivyopangwa vinafundishwa," alisema.

Pia alisema kuna mwamko mdogo wa wazazi ikiwamo kushindwa kuwawezesha chakula watoto mchana.

Alisema lengo la kongamano hilo ni kuwakutanisha wadau kutambua hali halisi na changamoto za elimu kwa Mkoa wa Dodoma na kuafikiana juu ya vipaumbele vya muda mfupi, wa kati na mrefu ili kuinua elimu mkoani hapa.

Sambamba na hilo, alisema katika kongamano hilo itazinduliwa kampeni maalum na endelevu ya uchangiaji wa jamii katika ujenzi na ukarabati wa miundombinu na samani za shule ili kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia.

"Tutaweka mikakati na kuamsha hamasa ya kujifunza na kutoa tuzo kwa walioonyesha kipekee. Ni kweli kuna baadhi ya maeneo Dodoma wanafanya vizuri na tutawatambua na kuwa chachu kwa wengine, kutakuwa na mdahalo wa kina," alisema.

Ofisa Elimu Mkoa wa Dodoma, Maria Lyimo, alisema mkoa huo umepanda kwa ufaulu kutoka asilimia 54 mwaka 2016 hadi 74 mwaka jana na kwa matokeo ya darasa la saba mwaka jana, ilishika nafasi ya 23 kitaifa na kidato cha nne nafasi ya 19.

# Wawekezaji wa Nigeria waitwa fursa Zanzibar

**Na Rahma Suleiman, UNGUJA**

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewakaribisha wawekezaji na wafanyabiashara kutoka Nigeria kuwekeza katika sekta yoyote wanayoitaka visiwani humo.

Aliyasema hayo alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Nigeria nchini, Dk. Sahabi Isa Gada, Ikulu mjini Unguja akiwa amefuatana na ujumbe wa wafanyabiashara na wawekezaji wa Kampuni ya IBRU ya Nigeria.

Dk. Shein alisema Zanzibar ina rasilimali nyingi za uwekezaji, hivyo ni vyema wafanyabiashara na wawekezaji hao wakaangalia sekta wanayoitaka na baadaye kutumia fursa hiyo ya kuwekeza.

Alisema kampuni hiyo ina uzoefu katika uwekezaji wa sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya uvuvi iliyowekeza ndani na nje ya Nigeria, hivyo ni vyema wakaangalia uwezekano wa kwenda kuwekeza Zanzibar katika sekta nyingine zilizoko.

Alisema juhudi kubwa zinachukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha sekta ya uvuvi ikiwa ni pamoja na kuifufua kampuni yake ya uvuvi iliyoanzishwa miaka ya 1970, lakini kunahitaji ushirikiano wa pamoja na kampuni zenye uzoefu katika sekta hiyo.

Rais Dk. Shein alimwambia Balozi huyo na ujumbe wake kuwa Serikali Zanzibar imeweka milango wazi kwa wawekezaji wanaotaka kwenda kuwekeza Zanzibar kwa kuwawekea mazingira mazuri kupitia Mamlaka ya Uwekezaji Vitega Uchumi Zanzibar (Zipa).

Alisema Zanzibar inahitaji viwanda vya uvuvi hasa ikizingatiwa kuwa imezungukwa na bahari ambayo ina rasilimali nyingi wakiwamo samaki wenye sifa za kipekee duniani.

Alisema uvuvi wa bahari kuu bado haujafanyiwa kazi ipasavyo kutokana na ukosefu wa vifaa, viwanda vya kuchakata samani na hata utaalamu wa uvuvi wa kisasa.

Dk. Shein alisema uvuvi ni sehemu ya uchumi wa Zanzibar na nchi yake haiko tayari kuachwa nyuma na ndiyo maana juhudi za makusudi zimekuwa zikichukuliwa na serikali anayoiongoza katika kuhakikisha inatekeleza vyema mchakato huo. Alisema imefika wakati kwa nchi za Bara la Afrika kuzidisha ushirikiano wa pamoja katika sekta za maendeleo na uchumi hasa ikizingatiwa kuwa Afrika ina utajiri mkubwa wa rasilimali.

Balozi wa Nigeria nchini, Dk. Gada, alisema ujio wa wafanyabiashara na wawekezaji hao kutoka Nigeria unatokana na mazungumzo aliyoyafanya kati yake na Dk. Shein wakati alipokwenda kujitambulisha Februari 28, 2018.

Balozi alisema miongoni mwa mambo matatu makubwa waliyozungumza ni pamoja na nchi yake kupeleka wawekezaji Zanzibar, jambo ambalo amelifanyia kazi.

Balozi Gada alisema wafanyabiashara na wawekezaji aliofuatana nao kutoka Kampuni ya IBRU, wana uzoefu mkubwa katika uwekezaji wa sekta mbalimbali na tayari wameshaekeza nchi kadhaa barani Afrika.

Alisema wawekezaji hao wamewekeza ndani na nje ya Nigeria katika sekta za uvuvi, mawasiliano, hoteli na utalii, kilimo, usafiri wa anga, mafuta na gesi asilia, usafiri na usafirishaji wa baharini pamoja na sekta ya habari.



Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale wa Zanzibar, Chumu Kombo Khamis, akichangia mada kuhusiana na taarifa ya kikao cha kwanza cha Mawaziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo wa Tanzania Bara na Habari, Utalii na Mambo ya Kale wa SMZ, mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Waziri avipa jukumu vyuo tatizo la ajira

**Na Mwandishi Wetu, UNGUJA**

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Riziki Pembe Juma, amewataka walimu wanaotoa mafunzo katika vituo vya amali, kuhakikisha wanatoa mafunzo yatakayowawezesha vijana kujiajiri na kukidhi soko la ajira nchini.

Akifungua juma la Mamlaka ya Mafunzo ya amali mjini Unguja juzi, waziri huyo alisema ni jambo la msingi kwa vituo hivyo kutoa mafunzo kwa kulenga kuwa na wahitimu wanaojiajiri wao wenyewe kwa kulipa kipaumbele somo la ujasiriamali.

Alisema mamlaka katika kuendeleza hilo, inatarajia kutoa fani nyingine mpya za usindikaji vyakula na ukarimu wa hoteli na fani za uvuvi na ufugaji wa ngombe katika vyuo vipya vilivyoko Makunduchi, Unguja na Daya, Pemba.

Waziri Riziki alisema kutokana na umuhimu wa mafunzo hayo, tayari serikali imeshajenga vituo viwili vya mafunzo hayo kikiwamo cha Mkokotoni, Kaskazini Unguja na Vitongoji, Kusini Pemba na wanamalizia kujenga vituo vingine viwili.

Alisema serikali bado ina mpango wa kuongeza vituo katika kila wilaya za Unguja na Pemba kwa lengo la kuhakikisha mafunzo hayo yanawafikia vijana wengi kwa Zanzibar na kulipatia ufumbuzi suala la ajira.

Alisema katika kuimarisha mafunzo hayo, serikali inawajengea uwezo walimu kutengeneza mitaala mizuri inayoendana na soko la ajira, kujenga na kuongeza majengo ya vyuo, kuziimarisha karakana za ufundi zenye mashine za kisasa pamoja na kuwapo kwa vifaa vya kujifunzia kwa nadharia na vitendo.

Aliwataka wazazi na walezi kuwapeleka watoto wao hasa wa kike ambao wamemaliza elimu ya lazima ili kupata ujuzi wa kujiajiri.

"Nawasisitiza sana hasa vijana wa kike, changamkieni fursa hii, kupata ujuzi wenu ambao utawawezesha kujiajiri na kuondoa mitazamo potofu kuwa mafunzo ya amali ni fani za kiume.

"Ni ukweli usiopingika kwamba ufundi ni silaha kubwa ya kuwafanya vijana wetu kujiajiri na kujipatia kipato cha halali," alisisitiza. Naibu Katibu Mkuu Taaluma wa Wizara hiyo, Madina Mjaka Mwinyi, alisema kuwapo kwa maonyesho hayo ni chachu ya kuvitangaza vituo hivyo ili jamii ielewe kazi za vyuo hivyo pamoja na kuvitumia ipasavyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Bakar Ali Silima, alisema dhamira ya kuadhimisha juma la mamlaka hiyo ni kuzitangaza kazi zinazofanywa na vijana katika vyuo vya amali.

Alisema wazazi watapata fursa ya kuona yale ambayo vijana wao wanafanya na kuendelea kuwaruhusu kujiunga na vyuo hivyo kwa lengo la kujiajiri.

# Bosi ZFDA akumbusha athari dawa, vipodozi

**Na Rahma Suleiman, UNGUJA**

MKURUGENZI wa Idara ya Dawa na Vipodozi ya Wakala wa Chakula na Dawa Zanzibar (ZFDA), Mposanje Lichanda, amewataka wafamasia na wananchi kuhakikisha wanadhibiti usalama na ubora wa dawa kwa matumizi ya binadamu ili kuepusha kutokea madhara kwa mtumiaji.

Aliyasema hayo kwenye Ukumbi wa Sanaa wa Rahaleo juzi alipofungua mkutano wa wadau wanaohusika na utafiti wa madhara yanayotokana na dawa na vipodozi pamoja na tiba za asili.

Alisema katika uchunguzi walioufanya, wamegundua uwasilishwaji wa matumizi ya dawa ni mdogo, hivyo usalama wa watumiaji wa dawa ni mdogo pia.

Alisema katika kudhibiti hilo, ZFDA inahitaji ushirikiano zaidi na wadau mbalimbali na watumiaji wa dawa hizo ili kuhakikisha dawa hizo zinakuwa salama kwa watumiaji.

Alisema kitaaluma, dawa zote huwa na madhara yake, iwe ya hospitali au ya miti shamba na matumizi yakizidi kiwango, yanakuwa na madhara makubwa zaidi.

"Wito wangu kwa jamii iache kula dawa bila kupata ushauri wa daktari ili kujiepusha kutokewa na madhara yanayoweza kujitokeza, tumezoea kujisikia kuumwa na kichwa, au uchovu ndani ya mwili unakula dawa bila ushauri wa daktari, tuache mara moja," alionya.

Mkurugenzi huyo alisema iwapo itatokea tatizo lolote kwa mtumiaji wa dawa, ni vyema kwenda katika hospital aliyopewa dawa na kutoa ripoti ili kufanyiwa uchunguzi na baadaye kupewa tiba nyingine.

Akiwasilisha mada katika mkutano huo, Mkuu wa Usalama na Ubora wa Dawa wa ZFDA, Mohammed Omar Simba, alisema katika matibabu, dawa zikitokea kuleta madhara kwa binadamu, itabidi zirekodiwe ili baadaye zishughulikiwe ili kutosababisha madhara zaidi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT



**KYLIE JENNER ATUMIA MILIONI 36 KULALA USIKU MMOJA** Soma UK.19

JUMAMOSI MACHI 7, 2020



CHOZI LA SONIA

# Laibua makandokando mengi, Aslay lawamani

BASI SAWA

## Hemed sema yote, sisi yetu macho

MWIGIZAJI wa filamu na mwanamuziki, Hemedy PHD, amesema yeye na Irene Uwoya ni watu wa karibu wanaosaidiana pesa pale mmoja anapohitaji.

Hemedy PHD amesema Irene Uwoya ni sehemu ya familia yake kwa sababu, wamekuwa wakisaidiana kuanzia ushauri, kula bata na kazi zingine.

"Irene Uwoya ni mwanangu tunasaidiana vitu vingi sana vya kimaisha, hata nikimwambia nimekwama atanilinda kuanzia ushauri, pesa, bata na kazi kwahiyo tupo karibu na kwangu ni zaidi ya familia, mara ya mwisho ilikuwa mwezi wa 6 mwishoni nilimpigia simu akanipa kama moja ya saba hivi" amesema Hemedy PHD.



## Busara za AY kwa wanaowasema vibaya wanawake

RAPA mkongwe nchini, AY, amewashauri wanaume kuwaongelea vizuri wanawake katika upande wa maisha yao na kuwahimiza kufanya kazi kwa bidii.

AY amesema watu wasiishie kuwasifia wanawake kuhusu mvuto, uzuri au urembo wao, bali wanatakiwa kuwahamasisha wanaweza kufanya mambo makubwa zaidi kuliko wanaume.

"Mara nyingi watu huwasifia wanawake kwenye upande wa pili wa mambo ambayo wanavutia au warembo, lakini itakuwa vizuri zaidi kama utawahamasisha na kujaribu kuwaonyesha kama wanaweza kufanya vitu vikubwa zaidi hata kama ni mwanamke" amesema AY





# Barua ya Idris Sultani kwa tasnia ya filamu

MSANII wa uchekeshaji Idris Sultan, ameonesha anavyoumia jinsi tasnia ya filamu inavyozidi kushuka na hakuna mtu aliyejitokea kuiokoa.

Idris katika ukurasa wake wa Twitter, ameandika barua akiwaomba watu kumpa nafasi ya kuinua sanaa hiyo kama watakuwa na imani naye.

"Ndugu zangu movies sio kama mziki, kwamba utaitwa stage ukaigize series yako ulipwe au utapiga 'tour' unaigiza kwenye majukwaa, kuna vipaji vingi sana mtaani ninavyojaribu kuvitengenezea njia, inaweza kuwa wewe au hata mtoto wako" ameandika.


"Ninachowaomba ni mniamini na mnipe nafasi nisukume hili gurudumu kwa ajili ya familia zaidi ya milioni ninazozijua, zitategemea kwenye hii njia ninayotengeneza, ahsante kwa upendo wenu na sapoti yenu" ameongeza.

## INSTA-TWITTER





**Jua** wakati sahihi wa kuanza biashara au mradi, kwani kwa kutojua wakati sahihi kutakupelekea kufanya kazi zako vibaya-**Mkude Simba.**



**Mwendo** wa kobe taratibu lakini anafika aendako. La msingi ni kutokata tamaa-**Kajala Masanja.**



# Dully Sykes ungethubutu sasa jela ingekuhusu

MSANII mkongwe wa Bongofleva, Dully Sykes, ameweka wazi kwamba ameachana na tabia ya kujihusisha kimapenzi na wasichana wadogo kwa umri wake unahitaji heshima.

Dully ameambia EATV na EA Radio, wakati ule alikuwa akipata kashfa hizo alikuwa ana umri mdogo kwa hiyo haikuwa shida kwake.

"Nilipokuwa mtu mzima nikaanza kuchukua watu wazima wenzangu hadi nikapata nao watoto kabisa na sijawahi tena kuchukua wasichana wa aina hiyo " amesema.

## UNASEMAAA...

# Z Anto mahaba hayo si bure

MWANAMUZIKi wa kizazi kipya, Z-Anto, amesimulia kisa cha kupotea kwake kwa muda mrefu, akisema alitokana na mrembo wake Binti Kiziwi kuhukumiwa kifungo nchini China.

"Tatizo kubwa ambalo lilimpoteza uraiani alikamatwa na madawa ya kulevya nchini China, akafungwa kwa takribani miaka nane ndiyo amekuja kukanyaga tena Tanzania mwishoni mwa mwaka 2019, japokuwa kila mtu alikuwa anaongea lake na wengine walikuwa wanatamani atoke" ameeleza Z-Anto.

Sandra Khan maarufu kama Binti kiziwi, alikuwa mke wake wa ndoa, lakini waliachana kwa sababu binafsi kabla ya kukamatwa miaka mitatu baadae.



## INSTA-TWITTER



**Wakati** mwingine kwenye uchumba kuna vijitabia unaviona havikupendezi lakini unajipa moyo atajirekebisha tukioana ...ndugu yangu havibadiliki hivyo..na mkianza kuishi kama mume na mke utaviona kero kuvivumilia.. hakuna tabia mpya utakayoiona inakuudhi kwenye ndoa ambayo hukuiona kwenye uchumba-**Jacob Steven JB.**



**Yaani** mkuu nataka nikwambie kwamba huyo Jackline Wolper huyo ndio bingwa wa kuonewa. Yaani nafatwa paka dukani na vigoma Tandika nitoe hela nilizotapeli. Mpaka kutishiwa kulogwa kwa kweli hao watoto ni tishio walishahuck mpaka namba yangu ya simu na insta. Jamani hawa vijana wa Mbeya sijui wanatumiaga nini, huyo mmoja aliniambia hawezi kukamatwa -**Jackline Wolper.**



**Mtoto** wa jirani anacho.. Akipita natoa macho.. Kile kidude ambacho... Kuna mtu anatamba nacho-**Tundaman.**

Kuumbe!





CHOZI LA SONIA

# Laibua makandokando mengi, Aslay lawamani

UKISIKIA sauti yake tu, utagundua kuwa ni mwanamke mpole, mwenye mahaba ya kweli na hulka za kike,

Mwanamke huyu si mwingine ni Sonia, ambaye ni mama mtoto wa mwanamuziki nyota nchini Aslay. Wawili hao wamejikuta wakiwa katika kizungumkuti ambacho wapambe wanahusishwa kuweka jambo hilo hadharani.

Ukimtizama usoni na kufuatilia maongezi yake ni wazi Sonia ana hulka za kike, ana aibu kiasi na si mtu wa kuweka wazi mambo yake binafsi.

Pamoja na urembo wake alijiona ufahari kuishi chini ya kivuli ili kutomletea kero mpenzi wake ambaye ni msanii maarufu katika ukanda wa Afrika Mashariki.

Wanawake wengine wana mambo mengi ya kujifunza kutoka kwa Sonia, si kwa kuonekana ni dhaifu, La Asha! Ila ni jinsi gani alivyokuwa tayari kumlinda mwanawe, kujishusha kulinda hadhi ya mwingine na pia kuomba msamaha pale alipoona amekosea.

Sakata liliibuka baada ya kurushwa video ambayo ilimuonesha ndugu wa Sonia wakilalamika mtoto wao kapigwa na Aslay kwa kosa la kwenda nyumbani kwake kuomba matunzo ya mtoto.

Katika mahojiano na Ayo TV, Sonia ameonesha ustaarabu na kukana yote akisema Aslay hakumgusa bali siku ya tukio kulitokea kurushiana maneno tu.

Baadhi ya watu watamuona mrembo huyo anajiosha kwa Aslay ili kumuosha, lakini ukweli utabaki kuwa kutokana na uso wake mtulivu na hulka ya upole ameamua kusema ukweli.

"Aslay hakunipiga, ila siku ile kulitokea kurushiana maneno baada ya kuniambia niondoke nyumbani kwake wakati hajanipa matunzo ya mtoto," amesema.

Sonia anasema yeye hana matatizo na mzazi mwenzake na kwamba anachotaka ni kumtunza mtoto katika malezi bora.

Amepinga dhana kwamba aliamua kuzaa na Aslay kwa kutaka umaarufu, akisema angetaka hivyo basi angetangaza mapema ujauzito wake na mtoto katika mitandao ya kijamii.

"Mimi sitaki umaarufu na sipendi na ndio maana niliamua kutotangaza ujauzito na mtoto hadi mgogoro huu ulipoibuka," amesema.

Ameeleza hata alipokutana na Aslay hakuwa na nia ya kujinufaisha binafsi, na ndio maana amekubali kuishi kwa shida katika nyumba za kupanga wakati wa ujauzito na hata alipojifungua mtoto wa nyota huyo.

"Chumba nilichopanga Aslay hahusiki kulipa pango, lakini mimi sijali hilo kwa sababu uhusiano wetu haukutokana na umaarufu wake au kuna kitu natafuta kwake, hapana tulipendana inatosha," ameongeza Sonia.

Ameeleza baadhi ya watu walimshauri aende kuishi kwa Aslay, lakini alikataa kwani lengo lake ni kuona mtoto anatunzwa na si yeye kujipeleka.

Sonia anamshukuru Meneja wa Aslay, Chambuso, kwa kusimama upande wake kila mara pale inapokea tatizo, hata hivyo anajutia kutomtaarifu suala hilo mapema kwani pengine angeweza kutoa msaada mapema.

Mama yake mdogo Sonia, Mama Trisha, amejitokeza na kueleza mtoto wake amewavua nguo kwa kuwakana hadharani kwamba hakupigwa.

"Sonia ametudhalilisha kwa kuikana familia yake, hili jambo limetuuma sana kwani mimi nisingejua kama amepigwa endapo asingenipigia simu yake.. huu ni mpango wa kutuvuruga ili amtetee Aslay," amesema.

Amesema tabia ya Sonia inawatia mashaka kwani licha ya mtoto aliyezaa na Aslay, ana wengine wanne ambao baba zao hawajulikani na wao anawakana.

"Sonia ana watoto watano, wengine wapo Zanzibar tunawalea lakini mwanetu anawakana eti ana mtoto mmoja, tunamtaka ajitokeze aje nyumbani kwa sababu ametukwaza kwa kiwango cha juu," amesisitiza.



# Wanamuziki walioibuliwa mikongeni

**Na Adam Fungamwango**

KABLA hata ya Uhuru wa Tanganyika, sehemu za Tanga kuanzia Hale kuelekea Tanga mjini kuna mashamba makubwa ya mkonge ambayo enzi hizo yalihitaji wafanyakazi wengi.

Watu kutoka mikoa ya ndani na nje ya nchi walimiminika kwenye mashamba ya mkonge kwa ajili ya kufanya kazi.

Kutokana na hali hiyo kulihitajika huduma za jamii kama zahanati, shule, baa na hata kumbi za burudani.

Hiyo ilisababisha wenye vipaji vya kupiga gita na kuimba, kuunda vikundi vya burudani. Bendi kama Atomic Jazz na Jamhuri Jazz ambayo awali ilijulikana kama Nyamwezi Jazz ziliibuka.

**WILSON PETER NA GEOGE PETER KINYONGA**

Wanamuziki hawa ndugu ni baadhi ya wanamuziki ambao wametokea maeneo ya Hale mkoani Tanga.

Asili yao ni Mkoa wa Kigoma na Rukwa walikotokea wazazi wao wakija kufanya kazi mikongeni.

Walitokea kuwa wanamuziki wakubwa Afrika Mashabiki, baada ya kuunda bendi ya Simba Wanyika nchini Kenya.

Kabla ya hapo walianzia Tanga kwenye bendi ya Jamhuri Jazz kwenye miaka ya '60, kabla ya kuelekea Arusha na kuvuka mpaka kuelekea Kenya ambako walipiga muziki kwa miaka mingi, wakafariki huko na kuzikwa huko mwanzoni mwa miaka ha '90.



TX

**TX MOSHI WILLIAM**

Ukimsikiliza Tx Moshi uimbaji wake, unafanana sana na George Peter wa Simba Wanyika. Ukweli ni kwamba Tx Moshi alimpenda sana mwanamuziki huyo na kuiga aina yake ya uimbaji.

Kwa mujibu wa Tx Moshi mwenyewe kabla hajafariki mwaka 2006, ni kwamba alicheza na George wakati wa utoto, huku Wilson akiwa mkubwa kidogo kwao.

Na wote walifundishwa muziki na mzee Mwanamasongi huko Hale mkoani Tanga. Kwa upande wake wazazi wake walitoka Mwanza na mama yake akitokea Ruvuma.

Baada ya kutoka mkoani Tanga, alikwenda Dar es Salaam na kujiunga na Polisi Jazz, kabla ya kuchukuliwa na Juwata Jazz Band 'Msondo Ngoma'.

**HAMZA KALALA**

Ni mpiga solo maarufu nchini. Wazazi wake wana asili ya Mkoa wa Katavi kwa sasa.

Walikwenda Tanga kwa sababu ya kazi za mikonge. Yeye amezaliwa huko na kujifunza muziki, kabla ya kuwa mwanamuziki mkubwa nchini, akipigia bendi mbalimbali kama Uda Jazz, Vijana Jazz, Matimila, Washirika na Bantu Group.

**HEMED MANETI**

Ni mwanamuziki mwimbaji maarufu nchini aliyefariki dunia mwaka 1990 jijini Dar es Salaam akiwa ni kiongozi wa bendi ya Vijana Jazz. Huyu naye ametokea mikongeni Tanga. Baba yake ni mzaliwa na Sumbawanga mkoani Rukwa na alikwenda huko na kufanya kazi ya udereva.

Alifundishwa muziki huko, lakini aliibukia mkoani Morogoro akiwa na Cuban Marimba, TK Lupopo na baadaye Vijana Jazz.



MANETI

**LUZA ELIAS**

Huyu ni mpiga saxophone maarufu nchini akitokea mkoani Iringa. Aliibuka kuwa mwanamuziki maarufu akiwa na bendi ya Jamhuri Jazz akiwa na kina Wilson Peter na George Peter na baadaye walimchukua kwenda naye Simba Wanyika, kabla ya kurejea nchini na kujiunga na Mwenge Jazz.



HAMZA KALALA

IMETOKEA

# Watu wagombea karatasi za chooni, maduka yatangaza kuwa tupu

UGONJWA wa Corona umesababisha mikasa na vituko vingi vya kushangaza wengi. Huko Australia mambo yamekuwa tofauti kwani karatasi za chooni zimepotea madukani baada ya watu kununua shehena yote.

Hivi sasa kila anayekwenda dukani kuulizia bidhaa hiyo, wanaambiwa hakuna kutokana na kununuliwa kwa wingi kwa kuhofia ugonjwa wa Corona.

Hata hivyo, serikali imekana kuwapo kwa uhaba wa karatasi hizo na kueleza zipo na zinatengenezwa kwa wingi.

Hata hivyo katika jiji la Sydney, ambalo ni kubwa zaidi wamiliki wa maduka wameamua kuuza kwa idadai ya karatasi nne pekee kwa mtu mmoja baada ya bidhaa hizo kufika kikomo.

Polisi waliitwa kwenye siku ya Jumatano, kumaliza mzozo baada ya mtu mmoja kutoa kisu ili kushinikizwa kuuziwa.

Kwenye mitandao ya kijamii kampeni ya hashtag ya #toiletpapergate na #toiletpapercrisis zilitamba. Karatasi hizo zilikuwa zikiuzwa kwa mamia ya dola mtandaoni, huku wasikilizaji wakipiga simu kwenye vituo vya redio ili kushinda vifurushi vya karatasi za chooni.

Hali inaonesha kuwa kulikuwa na ripoti ya watu kuiba karatasi za chooni kwenye vyoo vya umma.

Tatizo la uhaba wa karatasi za chooni si jambo geni, hali kama hiyo pia imejitokeza kwenye maeneo mengine yaliyoathiriwa na virusi vya corona kama vile Singapore, Japan na Hong Kong.

Mwezi uliopita, wanyang'anyi waliiba maburungutu ya karatasi za chooni huko Hong Kong kutokana na hali ya upungufu wa karatasi hizo.

Nchini Australia, hali hii ilianza mwishoni mwa wiki iliyopita baada ya kuripotiwa kwa kifo cha mtu mwenye maambukizi ya Covid-19.

Mpaka siku ya Jumatano, Australia imerekodi visa 41 vya maambukizi.

Mamlaka zimetaka watu kuacha kugombea bidhaa hiyo, na kupunguza uvamizi wa maduka wakieleza si suala la maana kufanya wakati huu.

Maduka makubwa kama Coles na Woolworths yameanza kuagiza bidhaa hiyo kwa wingi, huku wazalishaji Kleenex toilet paper nchini humo wanafanya kazi ya utengenezaji wa karatasi za chooni kwa saa 24 ili kukidhi mahitaji.





MAMU WA DAR

# Si kila king'aacho ni dhahabu

**Na Adam Fungamwango**

WASWAHILI wanasema kila king'aacho si dhahabu. Na wakati mwingine usiamini kila ukionacho kuwa kiko sawasawa. Fanya uchunguzi kwanza kwani unatakiwa kuwa makini kwa kila jambo unalotaka kulifanya.

Hakuna jambo rahisi kwenye dunia hii. Chochote kile kinachoonekana kuwa rahisi inabidi ukichuguze kwanza.

Wengi wameshatapeliwa kwa kupenda mteremko. Unapigiwa simu na kuambiwa kuna kazi, lakini utume pesa.

Unapigiwa simu unaambiwa umeshinda bahati nasibu, lakini hapo hapo unaambiwa kwanza namba yako lazima iwe na salio na ulitume. Na baadhi ya watu wanafanya hivyo bila kujiuliza kwanza.

Hapa duniani kuna hila nyingi za kutapeli watu pesa na wamekuwa wakitumia njia mbalimbali kila baada ya muda na wamekuwa wakifanikiwa kuwapata baadhi ya watu ambao wamekuwa hawajiongezi, au kupenda njia za panya au za mkato kupata utajiri, pesa, kazi, mapenzi na vingine vinavyofanana na hivyo.

Filamu ya 'Mamu wa Dar' inatuonyesha jinsi baadhi ya watu ambao wanapenda kuamini tu kila jambo na kutolichukulia tahadhari, kitu ambacho ni hatari kwenye maisha.

Imechezwa na Tini White, Ringo na wengineo.

Kwenye kijiji kimoja, anachoishi Ringo na Tini White anawasili msichana mmoja aitwaye Mariamu, akitokea jiji la maraha na karaha, Dar es Salaam.

Ni mwanamke aliyeumbwa akaumbika. Ameumbika kike haswa. Kwa sababu jina lake ni Mariamu, wakamkatisha jina wakamwita Mamu.

Umbile lake namba nane, mweupe, aliyejiongezea na mkorogo juu, urembo mwingine na mapambo, ukichanganya na utoto wa mjini, ulimfanya awe tofauti na wasichana na wanawake wengine wote kijiji hapo.

Wanaume wote kijijini hapo udenda ukawatoka. Wengi wakamtongoza. Wapo waliofanikiwa na wengine kumkosa. Wakati akipendwa na wanaume, alichukiwa mno na wanawake. Wengi waliona kabisa kuwa ndoa zao ziko mashakani.

Tini White alimtimua mkewe kwa sababu ya Mamu. Alitaka amuoe. Alikuwa ameshaonja asali anataka kuchonga mzinga. Kijiji kilitikisika haswa. Wanaume walishindana kutaka kumpata Mamu.

Hakuna hata mmoja aliyekaa na kujiuliza ni kwa nini amerejea kijijini kutoka Dar. Kwa nini msichana mrembo na mbichi kama yeye kuamua ghafla kurejea na kuanza maisha mapya kijijini, badala ya kuendelea kula raha za mjini.

Siku zikazidi kusonga mbele. Mamu akaanza kuumwa. Alichoumwa hakijulikani. Mama yake mdogo akaamua kumpeleka kwa mganga, lakini hali ilizidi kuwa mbaya.

Tini White kwa sababu yeye lengo lake ni kumuoa, alikwenda ukweni kutoa barua, lakini alimkuta Mamu mgonjwa, ndipo kwa gharama zake akaamua kumpeleka hospitali kwa ajili ya vipimo na matibabu.

Ikagunduliwa kuwa Mamu ameathirika na ukimwi. Inaonekana hata mwenyewe alijua na ndiyo maana aliamua kurejea kijijini, kwani kwa jinsi alivyo kama asingekuwa na tatizo lolote, angeweza kumtetemesha mwanaume yoyote wa mjini, achilia mbali kijijini.

Kijiji kilipata habari. Ikawa ni kilio na kusaga meno kwa wote waliotembea na msichana huyo akiwemo Ringo. Kila mmoja lilia kikwao. Baada ya matokeo hayo, Tini akaamua kujiondoa rasmi kwenye uchumba wa Mamu. Yeye hakuwa na wasiwasi kwa sababu hakuwahi kutembea naye. Alikuwa anataka amuoe moja kwa moja. Akaenda kumuangukia mkewe na kumhakikishia hajatembea na Mamu, tena kwa vipimo. Mkewe akakubali na kuanza maisha mapya.

Stori ya jiji ikabaki jinsi 'Mamu wa Dar' alivyochakaza kijiji kwa kuambikiza watu ukimwi.

KANYAGA HAPA UONE

# Kylie Jenner atumia mil. 36 kulala usiku mmoja



MWANAMITINDO na mjasiriamali kutoka familia ya Kardashian, Kylie Jenner, ametumia likizo yake akiwa katika hoteli ya kifahari iliyopo katika kisiwa maarufu cha Bahamas.

Kylie akiwa na mtoto wake Stormi na rafiki zake wa karibu, walikodi vyumba katika hoteli hiyo inayoitwa villa Rosalita, ambayo inaelezwa ni ghali na inapendwa na watu matajiri pekee.

Mrembo huyo ambaye kwa sasa anatambuliwa kama bilionea alitumia kiasi cha dola 15, 000 sawa na Sh. milioni 36 kulala kwa usiku mmoja ukiacha gharama zingine ambazo zipo nje ya huduma zao.

Hoteli ya villa Rosalita imejengwa karibu na ufukwe wa bahari ya Carribian wenye mchanga wa kupendeza.

Villa Rosalita inatofautiana bei zake kulingana na wiki na msimu, inaanzia kiasi cha dola 15,000 kwa usiku mwezi Mei 31 na kuanzia Juni kiwango chake ni 10,000.

Hoteli hiyo yenye vyumba 6 pekee vya kulala, kwa kawaida huwa imejaa wageni kutokana na kupendwa na watu wengi.

Ndani na nje ya hoteli hiyo imepambwa na mandhari nzuri ya miti ya maua, kuna bwawa la kuogelea, varanda kubwa inayotazama bahari na bustani ya kitropiki iliyozunguka maeneo ya maongezi.

Jengo la hoteli ina ngazi pacha zinazoelekea kwenye varanda mbili tofauti, sebule na chumba cha chakula chenye meza na vyombo vya kifahari.

Sehemu moja kuna chumba chenye samani za bei mbaya, dari zake zimenakshiwa rangi ya samawati na kuna michoro ya asili iliyochorwa ukutani.

Chumba cha daraja la kuu kuna mabomba yaliyonakshiwa mtindo wa Alfresco, na vyumba vingine vina milango tofauti ya kutoka kwenye varanda.

Kylie aliposti picha mbalimbali akiwa hotelini hapo na binti yake Stormi, pamoja na rafiki zake Anastasia Karanikolaou, Amber Asaly na wanawake wengine kadhaa.



# Hailey kumbe una maneno matamu

JE, umewahi kutumiwa ujumbe mtamu kutoka kwa mpenzi wako? Basi ujumbe wa Hailey Baldwin aliomtumia mume wake Justin Bieber, umekuwa gumzo kutokana na kuwa na hisia kali za kimahaba.

Justin Bieber wiki hii ametimiza miaka 26, ndipo mke wake Hailey alipoamua kumwandikia ujumbe mwanana kupitia ukurasa wake wa Instagram,

"Furaha ya kuzaliwa rafiki yangu kipenzi, asante kwa kuweka tabasamu kweye uso wangu kila siku...Nakupenda sana," aliandika Hailey.



## Mwigizaji mwingine mkongwe aaga dunia Nigeria

UNAWEZA kusema ni mwaka wa shetani kwa wasanii wa filamu wa Nollywood, kufuatia mfululizo wa vifo kwa wasanii wakongwe.

Safari hii msanii mwingine wa filamu wa siku nyingi, Kayode Odumosu, ambaye alijulikana kama Pa Kasumu, amefariki dunia.

Kifo cha Pa Kasumu, kilitangazwa na msanii mwingine wa Nollywood, Foluke DaramolaSalako ambaye alisema kabla ya kifo chake mwigizaji huyo alikuwa akisumbuliwa na matatizo ya muda mrefu.

## Rob Kardashian agonga mwamba

MAMBO yanamwendea kombo Rob Kardashian baada ya ombi lake la kutaka mahakama imkubalie kumlea binti yake kukataliwa.

Jaji huyo amekataa ombi la Rob la kumchukua Dream, kwa madai mama yake Blac Chyna, hawezi kumpa malezi yenye maadili.

Wakili wa Chyna amesema kwamba hatarudi nyuma katika azma yake ya kumzuia Rob na familia yake wasitekeleze azma yao hiyo

"Chyna ataendelea kuchukua hatua zote muhimu ili kuwalinda watoto wake, ikiwa ni pamoja na kumshinda Rob na familia yake kutaka kutokomeza furaha ya mteja wangu," imesema taarifa hiyo.







## Kumechafuka Nollywood kwa mipasho

NI mipasho kwenda mbele! Ndivyo inavyoonekana kwa wasanii wa filamu nchini Nigeria, Etinosa Idemudia na hasimu wake Victoria Inyama, baada ya wiki hii kukinukisha kwa kutumiana vijembe mtandaoni.

Katika majibizano hayo, Etinosa alimtupia kijembe Victoria kwa kumwambia hana jipya kwani amechanganyikiwa kwa kukosa kazi na mwanamke ajuza hasiye na mwelekeo.

Chanzo ni pale Victoria alipomtaka Etinosa kumuomba radhi baba yake wa kiroho kwa kumtoa ndani ya gari.

## Tonto usifanye hivyo, cha zamani huwa akiba

MWIGIZAJI nyota wa Nigeria, Tonto Dikeh, amemshukia aliyekuwa mume wake kwa kumuita mkabila na mbabe kiasi anajutia kukubali kufunga ndoa naye.

Tonto amesema mume wake huyo Churchill Olakunle ni mkabila.

Tonto Dikeh amefunguka hayo katika ukurasa wake wa Instagram na kuwashirikisha mashabiki wake kwa kuwauliza maswali wanajisikiaje kuolewa na mwanamume mbabe.

"Unaamka siku moja na unagundua umeolewa na mwanamume mkabila na mbabe, utafanya nini kujua kesho yako," aliuliza Tonto.



SAFU



MIONZI YA SHERIA

Na John Juma
0716217615

# Mpango wa matunzo ya watoto kwa wazazi waliotengana

BAADHI ya taarifa za msingi kuhusu jinsi mfumo wa sheria za familia zinafanya kazi kuhusu mipango ya uzazi wakati watu wanapoachana. Hazitolewi ushauri wa kisheria. Kama unafikiria kuachana au umeshaachana, unatakiwa kuomba ushauri wa kisheria kabla ya kufanya uamuzi kuhusu kitu cha kufanya.

Kutengana na watoto

Wakati unapotengana, mpenzi wako wa zamani atahitaji kufanya uamuzi muhimu kuhusu malezi ya watoto.

Sheria ya Familia ya 1975 ni sheria inayoonyesha kitu kinachotokea kwa familia zilizoachana kuhusu kutengana, mipango ya malezi, mali na utashi wa matengenezo.

Sheria inasema ni muhimu kwa watoto kuwa uhusiano mzuri na kila mzazi na watu wengine ambao ni muhimu katika maisha yao (kama mababu na mabibi), kama ni kwa ajili ya faida ya watoto na labda kama inawaweka watoto katika hasara ya kuumizwa.

Sheria inalazimisha wazazi kufanya juhudi za kutatua matatizo ya ulezi bila kwenda mahakamani. Wazazi wanatakiwa kufikia makubaliano kuhusu mipangilio ya watoto wao na jinsi ya kupata huduma ya kutatua matatizo ya kifamilia, kama vile upatanishi, ili kuwasaidia kufikia makubaliano.

Unyanyasaji wa majumbani katika uhusiano unaweza kuathiri jinsi sheria inavyofanya kazi. Ni muhimu kujulisha mwanasheria wako kama unahangaika, au umepatwa na vurugu za majumbani.

Kufanya mpangilio baada ya kuachana

Baada ya kuachana, ni muhimu kuangalia mpangilio wa kuishi wa watoto wako, ikijumuisha kiasi cha mda utakaotumiwa, na jinsi mtakavyowasiliana, ninyi kama wazazi. Ni muhimu kuangalia jinsi maamuzi ya mbeleni yatakavyotatuliwa kuhusu watoto.

**Usuluhishi ni mchakato ambapo wewe na mpenzi wako wa zamani mnaweza kujadili mipango kwa ajili ya watoto wenu. Hufanyika katika uwepo wa mtu anayejitegemea na asiyependelea aitwaye 'mpatanishi'. Mpatanishi hawezi kukushauri au kufanya uamuzi kwa ajili yenu, Kazi yao ni kuwasaidia wazazi kufikia makubaliano, kwa pamoja.**

Unaweza kuzungumza na mwanasheria ili kupata ushauri na msaada kuhusu mipangilio mnayoweza kuifanya. Wewe na mpenzi wako wa zamani mnaweza pia kuhudhuria suluhisho la mizozo ya familia kama vile upatanisho.

Suluhisho la mizozo ya familia na upatanishi

Usuluhishi ni mchakato ambapo wewe na mpenzi wako wa zamani mnaweza kujadili mipango kwa ajili ya watoto wenu. Hufanyika katika uwepo wa mtu anayejitegemea na asiyependelea aitwaye 'mpatanishi'. Mpatanishi hawezi kukushauri au kufanya uamuzi kwa ajili yenu, Kazi yao ni kuwasaidia wazazi kufikia makubaliano, kwa pamoja.

Wakati mkifikia makubaliano ambayo wote wawili mnayafurahia, yanaweza kuwa kumbukumbu kama 'mpango wa uzazi' au 'ridhaa ya maagizo'. Unapaswa kupata ushauri wa kisheria kabla ya kusaini mpango wa uzazi au maagizo ya ridhaa.

**Ridhaa ya Maagizo**

Ridhaa ya Maagizo ni mkataba ulioandikwa ambao hupitishwa na Mahakama. Una nguvu kisheria sawa na amri inayotolewa baada ya kesi kusikilizwa Mahakamani. Wewe na mpenzi wako wa zamani mnaweza kuomba ridhaa ya maagizo bila ya kwenda Mahakamani.

**Kwenda mahakani**

Kama makubaliano hayawezi kufikiwa, unaweza kuuliza Mahakama kuamua kuhusu mipango yenu ya uzazi

Kabla ya kwenda Mahakamani, wewe na mpenzi wako wa zamani mnatakiwa kuhudhuria suluhisho la mizozo ya famila, kama vile upatanishi.

Uhitaji huu wakati mwingine unaweza kuondolewa ikiwa kuna wasiwasi unaohusiana na vurugu za familia au unyanyasaji wa watoto.



KALAMU YA MWALIMU

Na Reubeni Lumbagala
0764-666349.

# Mkombozi wa mwanamke ni yeye mwenyewe

KESHO Tanzania inaungana na nchi yingine kote duniani kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani ambapo kwa mwaka huu, maadhimisho hayo yanaongozwa na kaulimbiu isemayo "Kizazi cha Usawa kwa Maendeleo ya Tanzania ya Sasa na Baadae".

Mwanamke ni mwanajamii muhimu katika kuleta maendeleo, bila mchango wake masuala mengi ya kimaendeleo yanakwama.

Uwepo wa maadhimisho hayo ni jitihada za Umoja wa Mataifa (UN) katika kuhakikisha changamoto kwa wanawake zinaondoka katika nyanja zote za kijamii.

Katika misingi hiyo mambo yanayomkwamisha mwanamke kiuchumi na kisiasa yanajadiliwa na kutafutiwa suluhisho la kudumu.

Kunatakiwa kuwepo na usawa wa kijinsia na kunufaika na fursa mbalimbali zilizopo katika jamii na nchi kwa ujumla.

Kwahiyo, Siku ya Wanawake Duniani sio siku ya kula, kunywa na kusherehekea peke yake, bali ni pamoja na kufanya tafakuri ya kina kuhusu mafanikio, changamoto za wanawake ili kufikia usawa wa kijinsia ambao ni muhimu katika maendeleo.

Somo ambalo Kalamu ya Mwalimu inalitoa kwa wanawake popote walipo hapa nchini ni kwamba kuelewa kuwa hakuna mafanikio kama wenyewe hawatashirikiana kwa pamoja kuhakikisha malengo yao yanafikiwa.

Mathalani, katika nyanja ya elimu, wasichana lazima watambue wao wenyewe ni askari wa kuwasimamia katika masomo na kwamba kama hawaoni umuhimu wa kusoma kwa ajili ya kujiletea ukombozi wa maisha, hakuna mwingine atayakaweza kuwasimamia.

Kama wanawake wanataka usawa wakijinsia huku wakipuuza umuhimu wa kusoma kwa bidii, hakutakuwa na namna ya kufikia badala yake watakuwa nyuma kielimu dhidi ya wanaume.

Katika siasa ni muhimu kwao wanashiriki katika kugombea nafasi mbalimbali za uongozi, na hili inategemea sana utashi wa wanawake kushiriki katika siasa bila kusubiri msukumo kutoka kwa wanaume.

Wanawake wenyewe waone umuhimu wa kugombea nafasi mbalimbali za kiuongozi ili lengo la kuwa na wastani wa asilimia 50 na wanaume litekelezwe.

Ikiwa wanawake watakosa uthubutu na kujiamini juu ya uwezo mkubwa walionao kiuongozi, wanaume wataendelea kushika nyadhifa mbalimbali wao wakiambulia nafasi za uteuzi.

**Somo ambalo Kalamu ya Mwalimu inalitoa kwa wanawake popote walipo hapa nchini ni kwamba kuelewa kuwa hakuna mafanikio kama wenyewe hawatashirikiana kwa pamoja kuhakikisha malengo yao yanafikiwa.**

Katika kuchangamkia fursa mbalimbali za kiuchumi,bado upo uzito wa wanawake kuziona na kuzitumia.

Wanawake wasisubiri kuletewa taarifa kuhusu uwepo wa mikopo inayotolewa na Halmashauri zote nchini, bali wao wenyewe wawe sehemu ya kufuatilia na waitumie katika kujiletea ukombozi wa kiuchumi.

Halikadhalika, zipo fursa za mikopo zinazotolewa na taasisi mbalimbali za fedha kwa ajili ya wanawake, hivyo wasisubiri kutangaziwa kuunda vikundi vya kukopeshwa, bali wenyewe waviunde na kuwasilisha taarifa zao katika taasisi husika.

Wanawake wanafanya kazi kubwa katika kushiriki shughuli za kilimo hapa nchini na kuchangia asilimia kubwa ya maendeleo ya nchi. Mafanikio haya ya ushiriki wa wanawake katika kilimo, yanapaswa kuonekana katika nyanja nyingine ili kukata kiu ya kufikia usawa wa kijinsia.

Upo umuhimu mkubwa wa wanawake wenyewe kutiana moyo ili wafanye mambo makubwa ya kimaendeleo bila kusubiri mchango wa wanaume.

Ni utamaduni mbaya wa kukatisha tamaa miongoni mwa wanawake na kupeana vikwazo katika kufikia malengo yai.

Mafanikio ya kutimia kwa kaulimbinu isemayo "Kizazi cha Usawa kwa Maendeleo ya Tanzania ya Sasa na Baadae" inategemea sana juhudi za wanawake wenyewe kujikomboa.

Hakuna namna ambayo nchi itafanikiwa katika hili kama wanawake wenyewe watabaki nyuma huku wakitegemea huruma na msaada wa wanaume kuwezeshwa.

Yote katika yote, wasichana na wanawake wasisahau wala wasipuuze umuhimu wa kusoma kwa bidiii kwani elimu ndiyo chemchem ya mafanikio.

Reubeni Lumbagala ni Mwalimu wa Shule ya Sekondari Mlali,Wilaya ya Kogwa, Dodoma.

*Maoni (+255) 765 409249.*

## CLARA ZETKIN

# MWANZILISHI WA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI



Na Mwandishi wetu

IDADI kubwa ya watu wanafahamu maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, yanayofanyika kila ifikapo tarehe 8 mwezi Machi.

Kabla ya tarehe husika wanawake wanatumia majukwaa mbalimbali kupaza sauti zao katika kukemea na kushinikiza uondowaji wa vikwazo vinavyowakwamisha kutimiza ndoto zao katika Nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii.

Maadhimisho hayo ambayo yanatambuliwa na Umoja wa Mataifa (UN) yanafanyika duniani kote katika kauli mbiu moja.

Je, unafahamu kwa nini dunia inaadhimisha siku hii? Na lini iliidhinishwa Machi 8 kuwa siku maalum kwa Wanawake?

Makala hii itakupa chimbuko la Siku ya Wanawake Duniani na wapi kulikuwa sehemu ya mwanzo kuadhimishwa.

**MAADHIMISHO YALIANZA LINI?**

Siku ya Wanawake Duniani ilianza mwaka 1908 baada ya wanawake 15,000 walipoandamana mjini New York nchini Marekani wakidai kupunguziwa muda wa kufanya kazi, ongezeko la malipo ya ajira na haki ya kupiga kura.

Hata hivyo, iliwachukua muda wa mwaka mmoja pale chama cha kisoshalisti nchini humo kutangaza siku hiyo ni kitaifa ya wanawake.

Lakini wazo la siku hiyo iwe ya kimataifa lilianzishwa na mwanamke anayeitwa Clara Zetkin, raia wa Denmark.

Mwaka 1910 alipendekeza katika mkutano wa kimataifa wa wafanyakazi wanawake huko Copenhagen Denmarkm kuweapo na siku maalum ya kutambua mchango wa mwanamke pamoja na kujadili changamoto zinazomkabili.

Katika mkutano huo uliwakusanya wanawake 100 kutoka nchi 17, wazo hilo walikubaliana nalo.

Kwa mara ya kwanza ilisherehekewa mwaka 1911, nchi nne zilihusishwa ikiwamo Austria, Denmark,Ujerumani na Switzerland.

Mwaka huu itakuwa maadhimisho ya 107 baada ya sherehe ya kutimiza miaka 100 kufanyika mwaka 201.

Tarehe 8 mwezi Machi haikuwa tarehe rasmi iliyopendekezwa na Clara Zetkin la, kwani Siku ya kimataifa ya wanawake duniani haikuwa na tarehe maalum na haikuwa rasmi mpaka kipindi cha vita ya mwaka 1917.

Wakati huo wanawake wa Urusi waliandaa mgomo na maandamano wakidai amani na kulalamikia upungufu wa chakula. Katika maandamano hayo waliimba wanataka 'Amani na Mkate'.

Siku nne za mgomo, zilifanya watawala wa Urusi kuwapa wanawake haki ya kupiga kura. Tarehe ambayo mgomo ulianza ulikuwa kwenye kalenda ya Julian, ambayo ilikuwa ikitumika nchini humo . Kumbukumbu inaonesha ilikuwa siku ya Jumapili tarehe 23 Mwezi Februari.

Siku hiyo katika kalenda ya Gregoria ilikuwa tarehe 8 mwezi Machi ambayo inaadhimishwa hivi leo.

**MAADHIMISHO TOFAUTI**

Siku ya kimataifa ya wanawake ni siku ya mapumziko katika nchi nyingi, siku hiyo mauzo ya maua huongezeka mara dufu kuanzia siku tatu au nne kabla ya kilele chake.

Katika kipindi hicho wanaume na wanawake huwapa zawadi ya maua wapendwa wao wa kike na wafanyakazi wenzao kama ishara ya kuwathamini.

Lakini nchini China, siku hiyo wanawake wengi hufanya kazi nusu siku kama ilivyoshauriwa na Baraza la nchi hiyo ingawa waajiri si mara zote wanatekeleza utamaduni huo.

Huko Italia, siku ya kimataifa ya wanawake au inafahamika kama 'La Fiesta della Donna' inasheherekewa kwa kupeana maua, chanzo cha utamaduni huu hakifahamiki lakini inaaminika ilianzia Roma baada ya vita ya pili ya dunia.

Nchini Marekani, Mwezi Machi ni mwezi wa historia kwa wanawake. Rais hutoa hutuba kila mwaka kuthamini mafanikio ya wanawake wa Marekani.

Mwaka huu siku hiyo inaadhimishwa kwa Kauli mbiu inayosema 'Usawa kwa Wote' ikiangazia usawa wa kijinsia.

Maadhimisho hayo yameleta matokeo chanya katika ustawi wa jamii duniani, wanaharakati wa kutetea haki za wanawake walipiga hatua kubwa.

Mwaka 2017, mamilioni ya wanawake walianza kampeni ya kupinga unyanyasaji na dhuluma za kingono katika mitandao ya kijamii.

Mwaka In 2018, kampeni yenye jina la #MeToo ilipata umaarufu, huku mataifa kama vile India, Ufaransa, China, na Korea Kusini yakijiunga na kampeni hiyo kushinikiza mabadiliko.

***Makala kwa msaada wa mtandao***

## MAKALA




Ofisa Maendeleo ya Jamii, Wilaya ya Ilala, Francisca Makoyo, akizungumza kwenye maadhimishio hayo.

### KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI...

# DAR WATAKA HATUA KALI KWA WAKEKETAJI

**Na Sabato Kasika**

MAADHIMISHO ya Siku ya Wanawake Duniani yanafikia kilele chake kesho, kuna mijadala mbalimbali ikiendelea ndani ya jamii kuangalia na kutafakari changamoto zinazowakumba watoto wa kike na wanawake.

Jumanne wiki hii vituo vya Taarifa na Maarifa kutoka baadhi ya kata za wilaya ya Ilala jijini Dar es Salaam, viliandaa kongamano lilofanyika kwenye viwanja vya Mahita, Kata ya Kipunguni kujadili vikwazo dhidi ya makundi hayo.

Katika tukio hilo ililohusisha Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), ajenda mbalimbali za maendeleo ya mwanamke zilijadiliwa, lakini washiriki wakajikita zaidi kujadili suala la ukeketaji unaofanyika kwenye maeneo yao.

Hii ni dhairi kwamba sasa jamii inazidi kuchukia vitendo vya ukatili wa kijinsia hasa ukeketaji, ambao umeathiri watoto, wasichana na wanawake kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Kutokana na hali hiyo, wanaitaka serikali kuendelea kumulika maeneo hayo ili kuhakikisha vitendo vya ukeketaji vinakoma na kuwafanya wawe salama.

Selemani Bishagazi ni Mkurugenzi wa Kituo cha Taarifa na Maarifa cha Kipunguni, ambaye anasema, jamii imechoka vitendo hivyo, ni vyema maeneo



Baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Ilala wakiwa kwenye maadhimisho hayo.

yenye ukeketaji yakashughulikiwa.

"Tunafanya kazi kubwa usiku na mchana kufuatilia vitendo hivyo na kutoa taarifa kwa mamlaka husika, lakini changamoto ni kubwa hasa kutokana na ukweli kwamba wahusika wanafanya kwa siri," anasema Bishagazi.

Anasema, anajua kuwa Desemba mwaka huu ni msimu wa ukeketaji, wanaomba juhudi zianze kufanyika kuhakikisha hakuna mtoto wala msichana atakayekeketwa.

Naye mkazi wa Kipunguni, Kisiri Nyagwisi anataka zifanyike kampeni za kukataa kuoa wanawake waliokeketwa kama njia mojawapo ya kupinga vitendo vya ukeketaji.

"Mimi ni mkurya, lakini sina mpango wa kuoa mwanamke aliyekeketwa, hivyo ninawashauri vijana wenzangu kuungana nami katika hilo ili tusaidie kukomesha ukeketaji nchini," anasema Nyagwisi.

Kijana huyo anatoa ushuhuda kwamba, aliwasaidia wadogo zake huko Tarime mkoani Mara, wasikeketwe kwa kuwapeleka katika kituo cha kulelea wasichana wanaokimbia vitendo hivyo.

Mgeni rasmi katika maadhimisho hayo, alikuwa Ofisa Maendeleo ya Jamii Wilaya ya Ilala, Francisca Makoyo, ambaye anawataka wananchi kusaidiana kupambana na vitendo hivyo.

Kuna Kamati ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA) ambazo zina mafunzo ya namna kutekeleza majukumu yake, shirikianeni nazo," anasema.

Anasema, lengo la uanzishaji wa kamati hizo kila halmashauri ni kutokomeza kabisa ukatili dhidi ya wanawake na watoto kuanzia ngazi ya kaya, kijiji, hadi kufika ngazi ya taifa.

"Tuzitumie vizuri ili kusaidia kutokomeza vitendo hivyo kwenye maeneo yenu na pia chagueni viongozi watakaokuwa na jukumu la kufuatilia na kutoa taarifa za vitendo hivyo," anasema Makoyo.

Makoyo anasema, kwa kufanya hivyo, mpango wa taifa wa kutokomeza matukio ya ukatili kwa wanawake na watoto unaweza kufikiwa na hivyo kulifanya kundi hilo kuwa salama.

Kwa upande wake Ofisa Progamu Mwandamizi wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Deogratius Temba, anasema usiri kwenye baadhi ya jamii bado ni tatizo linalochangia kuendelea kuwapo kwa vitendo hivyo.

"Umefika wakati sasa jamii ijadili kwa uwazi na kuwataja wale wote wanaofanya vitendo hivyo ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yao na pia wekeni ulinzi ili kuwalinda watoto wa kike," anasema Temba.

Anasema, ni muhimu jamii kujua namna ya kutoa taarifa za matukio ya ubakaji, ulawiti, ukeketaji na vipigo tena kwa wakati bila woga, vinginevyo matukio ya aina hiyo yataendelea kuwapo.

"Wanawake wanatakiwa kuwa katika mazingira salama ili waweze kukua kiuchumi, hivyo ni muhimu ziundwe kamati kwenye mitaa ambazo zitakuwa zinatoa taarifa za ukatili wa kijinsia," anasema.

Anafafanua kuwa taarifa hizo zinatakiwa kutolewa kwenye kamati ya maendeleo ya kata ili kutokomeza ukatili huo na kwamba TGNP iko tayari kuzijengea uwezo kamati hizo.

Wataalamu wa afya wanasema, ukeketaji unakwamisha utendaji kazi wa asili wa mwili wa mwanamke na una madhara makubwa kiafya, kisaikolojia na kiuhusiano.

Wanasema kuna madhara ya muda mfupi kama kifo kutokana na kutoka damu nyingi na maumivu makali, uharibifu mfumo wa nje wa viungo vya uzazi na maambukizi.

Vilevile wanasema, kuna madhara ya muda mrefu kama maumivu makali ya muda mrefu, maambukizi yakiwamo ya mara kwa mara ya njia ya mkojo, kupungua kwa raha ya kujamiiana.

Madhara mengine ni ya kisaikolojia, kama vile msongo wa mawazo utokanao na maumivu, kuongezeka kwa hatari za kujifungua kwa njia ya upasuaji na kuongezeka kwa vifo vya uzazi.

Mbali na hayo, madhara mengine ni kuongezeka kwa hatari za vifo vya watoto wachanga, kuongezeka kwa hatari ya watoto kuzaliwa kabla ya muda, kutokwa damu nyingi wakati na baada ya kujifungua.

MAKALA

# WANAWAKE SINGIDA WAOMBA ULINZI KWA WATOTO WA KIKE

**Na John Mapepele, Singida**

TAREHE 8, Machi 2020, Tanzania itaungana na nchi nyingine ambazo zinaadhimisha Siku ya Wanawake Duniani.

Kwa upande wa Tanzania maadhimisho ya siku hiyo yanaanza tarehe 5 Machi, kwa kufanyika shughuli mbalimbali za wanawake na wadau wake katika viwanja vya Halmashauri ya Mji wa Bariadi, mkoani Simiyu na kilele kitakuwa kesho huku mgeni Rasmi anatarajiwa kuwa Makamo wa Rais, Samia Suluhu Hassan.

Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto inasema kauli mbiu ya kitaifa ya maadhimisho ya siku hiyo kwa mwaka huu ni "Kizazi cha Usawa kwa Maendeleo ya Tanzania ya Sasa na Baadae"

Kwa mujibu wa Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) siku ya wanawake duniani imeanzia kwenye harakati za ajira hadi ilipokuja kutambuliwa na Umoja wa Mataifa kuwa siku maalum ya kuadhimisha katika mwaka.

Siku hii imekuwa ikipata umaarufu mkubwa huku nchi mbalimbali duniani zikija na mtindo mipya ya kuadhimisha, Serikali ya Tanzania kwa mfano katika mwaka huu, ilielekeza maadhimisho yaendelee kufanyika kuanzia kwenye ngazi ya mkoa ili kutoa wigo mpana kwa wanawake wadau mbalimbali na kila Mtanzania kutathmini hatua tulizofikia kama Taifa katika masuala ya usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake na wasichana.

Kanda ya kati ambayo imejumulisha mikoa ya Dodoma, Tabora na Singida maadhimisho hayo tayari yameshafanyika kwenye Mkoani Singida chini ya uenyekiti wa Mkuu wa Mkoa, Dkt. Rehema Nchimbi.

Awali, akifungua kongamano hilo Dkt. Nchimbi alisema usawa wa jinsia na haki za wanawake ni msingi wa maendeleo duniani na kusisitiza kuwa serikali inataka kuhakikisha inatokomeza ukatili wa aina zote ili kufikia malengo ya kuwa na kizazi chenye usawa kati ya wanaume na wanawake.

Amesema lengo la maadhimisho ya siku hiyo ni kutathimini utekelezaji wa atua za kufikia usawa wa jinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi, kijamii, kisiasa kwenye kufikia maendeleo jumuishi.

Aidha, amesema hatua hiyo ni chachu ya kuleta usawa wa kijinsia na maendeleo pamoja na kutokomeza kila aina ya ubaguzi, udhalilishaji na ukatili dhidi ya wanawake.



Dkt. Nchimbi, ameeleza maadhimisho hayo yanatoa fursa ya kuelimisha jamii kuhusu jitihada mbalimbali zinazofanywa na jamii, Serikali, Asasi za kiraia, Sekta Binafsi na wadau wengine katika kukuza hali ya mwanamke wa Kitanzania.

Kabla ya tathmini kufanyika mada mbalimbali ziliwasilishwa na wataalam kuhusu hali halisi ya takwimu za vitendo vya ukatili wa kijinsia nchini kati ya mwaka 2016/18, takwimu zinaonyesha vitendo hivyo vinazidi kuongezeka hapa nchini.

Juliana Ntukey, Ofisa Maendeleo ya Jamii kutoka Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, alionesha kuwa Mwaka 2016 idadi ya matukio ya unyanyasaji yaliyoripotiwa yalikuwa 31,996 na 2018 yaliongezeka na kufikia 43,487. Mikoa sita iliongoza kwa matukio hayo ni Dar es Salaam, Morogoro, Singida, Dodoma, Tanga na Arusha.

Aidha kosa la ubakaji na shambulio la kudhuru mwili ndiyo yameongoza kuwa na idadi kubwa ya waathirika ukilinganisha na makosa mengine.

Mwaka 2016 hadi 2018 kwenye kosa la shambulio la kudhuru mwili walikuwa 26,840 na ubakaji waliripotiwa waathirika 23,310.

Kwa mujibu wa takwimu za mikoa, Mwaka 2016 Temeke iliongoza makosa ya kijinai (4, 101), Morogoro (3,073), Singida (2,567), Arusha (2,890) na Tanga (1,904), huku mwaka uliofuata Kinondoni iliongoza wa matukio (7,854), Dodoma (3,927), Temeke (3,163), Singida (2,890) na Arusha (2,790).

Mwaka 2018 mkoa ulioongoza kwa matukio ya ukatili wa kijinsia na unyanyasaji ulikuwa Kinondoni (5,386), Temeke (3,999), Arusha (3, 904), Tanga (3,252), Dodoma (1,882).

Huku idadi ya watoto waliofanyiwa ukatili wa kijinsia katika kipindi hicho ikiongezeka kutoka 10, 551 mwaka 2016 hadi kufikia 14, 491 mwaka 2018. Takwimu zinaonyesha idadi ya watoto wa kike ni kubwa na imekuwa ikiongezeka kila mwaka ikilinganishwa na wale wa kiume.

"2016 watoto wa kike walioripotiwa kufanyiwa ukatili walikuwa 8, 496 huku wa kiume wakiwa 2, 055, mwaka 2017 wakike walikuwa 9,810 wakiume wakiwa 3647, na mwaka 2018 watoto wa kike walikuwa 11, 789 huku wa kiume wakiwa 2, 702," anasema Ntukey

Naye Ofisa maendeleo ya Mkoa wa Singida, Jonathani semiti katika mada yake ya Wanawake na fursa za uongozi anasema kuwa Wanawake ni wengi na ni jeshi kubwa inapaswa kutumia wingi wao kuwachagua ili waingie kwenye ngazi mbalimbali za uongozi.

Pamoja na mambo mengine, inapendekezwa kuanzishwa kwa vikundi huru vya wanafunzi kujadili masuala ya ukatili kwa wanawake kwenye maeneo ya shule zote katika mikoa ya Dodoma, Singida na Tabora ambavyo vitasimamiwa na walimu wa shule husika.

Lengo la vikundi inaelezwa kuwa ni kupeana elimu na kuhamasishana juu ya masuala yote yanayohusu ukatili na hatua zinazopaswa kuchukuliwa punde tu tukio hilo linapojitokeza miongoni mwa mtoto yeyote.

"Watoto wengi hukosa uhuru wa kuwaeleza wazazo wao matatizo yanayowapata ambapo wahanga wengi wanagundulika kuwa wamebakwa na kulawitiwa baada ya muda mrefu kupita," anasema Stella Mwagoha mmoja wa washiriki wa kongamano hilo kutoka Kituo cha Msaada wa Sheria kwa Wanawake na Watoto cha Faraja kilichopo Mjini Singida

Anaongeza kuwa watoto wanaendelea kukaa kimya wakiteseka ndani kwa ndani kwa maumivu makali, hatimaye inapita muda mrefu hana wa kumweleza, kutokana na wazazi wanautumia muda wao mwingi kwa kutafuta maisha.

Amina Abdallah amependekeza Serikali iwachukulie hatua kali wazazi wanao waozesha watoto wa kati ya umri wa miaka 13 na 14 kwa tamaa ya mali. Akasisitiza kinafanyika kwenye ndoa hiyo ya utotoni ni ubakaji, na wengi wa watoto hao walishindwa hata kumaliza darasa la saba.

"Kamati za ulinzi wa mtoto dhidi ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa watoto, wazee, wanawake na wenye ulemavu kuanzia ngazi ya taifa hadi vijiji zinafanya kazi kwa kusuasua kutokana na ufinyu wa bajeti," anaongeza Hellen Mtaita kutoka Dodoma, huku akishauri Serikali kuziimarisha Kamati husika

Aidha, ameshauri kuwapo na mpango mkakati kila Mkoa kutoa takwimu za hali halisi ya matukio ya ukatili na mwelekeo wake, ili kuangalia namna bora ya kupunguza kama siyo kutokomeza kabisa matukio hayo.

Kwa upande mwingine,Mkuu wa Mkoa wa Singida, Dkt. Nchimbi amezindua Jukwaa la Mkoa la Haki ya Jinai la Mkoa wa Singida ili kusaidia kupambana na uhalifu wa kijina na ukatili kwa watoto na wanawake.

Dkt. Nchimbi amesema kuzinduliwa kwa Jukwaa hili kutakuwa nguzo kuu ya kuzima uhalifu katika Mkoa wa Singida, huku akiwataka wajumbe kutumia jukwaa hili kufanya utafiti na kutafakari kwa kina ni namna gani bora ya kudhibiti uhalifu badala ya kusubiri utokee.

## Wahamiaji wakabiliana tena na polisi wa Ugiriki

**ATHENS,** Ugiriki

MAKABILIANO yamezuka tena leo kwenye mpaka wa Ugiriki na Uturuki, baada ya polisi wa Ugiriki kutumia gesi ya kutoa machozi na risasi za maji kuzuia jaribio la wahamiaji kuvuka mpaka kwa nguvu.

Askari wa Uturuki walijibu hatua hiyo kwa kufyatua mabomu ya machozi kuelekea upande wa mpaka wa Ugiriki.

Maelfu ya wakimbizi wamekuwa wakijaribu kuingia Ugiriki kupitia eneo la mpaka wa kusini kwa wiki kadha zilizopita, baada ya Rais wa Uturuki, Recep Tayyip Erdogan kutangaza mipaka yake na Ulaya iko wazi. Uamuzi wake wa kufungua mipaka ulikuja baada ya mashambulizi makali ya serikali ya Syria katika jimbo la Idlib, ambako vikosi vya Uturuki vinapambana. Mapigano hayo yamewaua wanajeshi kadhaa wa Uturuki na kusababisha raia karibu milioni moja wa Syria kukimbilia mpakani. **DW**



## Brazil yawaondoa wanadiplomasia wake Venezuela

**BRASILIA,** Brazil

SERIKALI ya Brazil imewaondoa wafanyakazi wake wa kidiplomasia kutoka nchini Venezuela, hatua hiyo ilitangazwa juzi Alhamis.

Uamuzi huo unaathiri ubalozi wa Brazil mjini Caracas, pamoja na balozi nyingine ndogo zilizoko kwenye miji mingine, kulingana na taarifa iliyochapishwa kwenye gazeti la serikali.

Hatua hiyo inadhihirisha kuendelea na mvutano kati ya Rais wa Brazil mwenye siasa za mrengo wa kulia Jair Bolsonaro na kiongozi Venezuela Nicolas Maduro.

Rais Bolsonaro alimtambua mjumbe anayemwakilisha kiongozi wa muda wa Venezuela aliyejitangazia madaraka, Juan Guaido, kama balozi wa Brazil.

Guaido alijitangaza mwenyewe kama rais wa mpito mwaka jana na anatambuliwa kama kiongozi halali wa Venezuela na mataifa zaidi ya 50 duniani. **DW**

# Marekani haina vifaa vya kutosha kupima corona

**WASHINGTON,** Marekani

IKULU ya Marekani imethibitisha kuwa nchi hiyo haina vifaa vya kutosha vya kupima virusi vya corona wakati viwango vya maambukizi vikiendelea kuongezeka.

Makamu wa Rais, Mike Pence, amesema utawala wa Trump hautaweza kufikia malengo yake ya kutoa vifaa milioni moja vya kupima virusi hivyo ndani ya wiki hii.

Wakati huo huo, bunge la Marekani limeidhinisha kwa haraka kupatikana kwa vifaa hivyo kwa dharura ili kukabiliana na mlipuko wa corona.

Katika matukio ya hivi karibuni zimethibitisha zaidi ya watu 92,000 wameambukizwa katika nchi mbalimbali duniani.

**Watu tisa wamefariki nchini humo kufikia jana na wote walikuwa wamezuiliwa katika kituo kimoja cha afya viungani mwa Seattle.**

Watu zaidi ya 80,000 wameripotiwa kuwa nchini China, ambako ni chimbuko la virusi hivyo.

Katika idadi hiyo, watu 3,000 wamefariki kutokana na ugonjwa huo. Idadi ya vifo vilivyotokana na virusi ya corona nchini Marekani imeongezeka hadi 12 siku ya Alhamisi, wagonjwa wengi wakiwa katika jimbo la kaskazini magharibi la Washington.

Kufikia jana zaidi ya watu 200 wamepata virusi vya Covid-19 katika majimbo 20 ya Marekani.

Katika jimbo la Washington, maofisa katika eneo la Seattle, wametangaza watu 20 kuambukizwa virusi vya corona, na kufikisha 70 kwa mujibu wa idara ya afya katika jimbo hilo.

Watu tisa wamefariki nchini humo kufikia jana na wote walikuwa wamezuiliwa katika kituo kimoja cha afya viungani mwa Seattle.

Baadhi ya kampuni kubwa katika eneo hilo, ikiwamo Microsoft na Amazon, yamefunga huduma zao au kuwashauri wafanyakazi wao kufanya kazi wakiwa nyumbani.

Viwango vya maaambukizi mjini New York viliongezeka mara mbili katika usiku mmoja na kufikia 22, wote kutoka mji huo au miji iliyo karibu. **BBC**



Profesa Silvio Franzetti wa kitivo cha Uraia na Mazingira wa Chuo Kikuu cha Polytechnic katika mji wa Milan, kaskazini mwa Italia, akiwa peke yake darasani baada ya wanafunzi wote kutakiwa kukaa majumbani mwao hadi Machi 15 mwaka huu, kuhofia kusambaa kwa virusi vya Corona. **PICHA: EPA-EFE**

# Kifo mlinzi wa Makamu wa Rais Kenya chazua utata

**NAIROBI,** Kenya

UTATA umeibuka kuhusu mazingira ya kifo cha Sajini Kipyegon Kenei, aliyekuwa Mkuu wa Usalama katika ofisi ya Naibu Rais wa Kenya, Dk. William Ruto.

Kifo hicho kimeleta maswali mengi kuliko majibu baada ya idara inayochunguza uhalifu (DCI) kudai kwamba kuuawa kwake kunahusiana na matukio katika ofisi ya kiongozi huyo.

Mkurugenzi wa Idara ya upelelezi, Gorge Kinoti, amesema kwamba Sajenti Kemei aliuawa kikatili, kinyume na taarifa za awali kwamba alijiua mwenyewe.

Mwili wa Kenei ulipatikana nyumbani kwake wiki mbili zilizopita ukiwa na jeraha la risasi.

Kifo cha askari huyo kilitokea wakati alitakiwa kuandika taarifa ya maelezo kwa polisi kuhusu washukiwa wa sakata la zabuni hewa ya ununuzi wa silaha za mamilioni ya pesa walipotembelea ofisi ya Dkt Ruto mjini Nairobi.

Kifo cha Kenei kimezua mjadala mkali nchini humo huku baadhi ya watu wakisema huenda aliuawa mahali tofauti na mwili wake ukapelekwa nyumbani kwake kwa lengo la kuficha ukweli.

Kabla ya mwili wake kupatikana, ofisi ya Dkt Ruto ilikuwa imetoa taarifa ikisema kwamba alikuwa ametoweka.

Wakenya hawakuridhishwa na hatua ambazo ofisi ya Dkt Ruto ilichukua na kukosoa hatua ilizochukua baada ya kushindwa kufika kazini alipotakiwa na wapelelezi kuandika taarifa.

Mkuu wa Upelelzi wa Kenya, DCI George Kinoti alisema awali kwamba, Sajenti Kenei alitakiwa kuandikisha taarifa polisi kueleza jinsi aliyekuwa waziri wa michezo, Rashid Echesa na washukiwa wengine wanne walivyowaingiza raia wa kigeni katika ofisi ya Ruto, na kutia sahihi kandarasi feki ya kuuzia wizara ya ulinzi silaha.

Kinoti ambaye alionyesha wanahabari picha zilizochukuliwa na kamera za CCTV, Sajini Kenei anaonekana akiwafungulia mlango na kuwaelekeza Echesa na ujumbe wake katika ofisi ya Naibu Rais.

Echesa, ambaye ni rafiki wa karibu wa Ruto, ameshtakiwa kwa kujaribu kujipatia dola za Marekani 395, 442,000 kutoka kwa wafanyabiashara wa Poland kwa kuwaahidi zabuni ya kuiuzia idara ya ulinzi ya Kenya vifaa vya kijeshi. **BBC**

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote. Afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo.

Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

# MAUAJI HARUSINI-3

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

KATIKA hali isiyo ya kawaida, mwaka mmoja baadaye Grace alikatisha mawasiliano na mpenzi wake Abesh.

Baada ya kumtafuta na kukusanya taarifa huku na huko, akagundua kuwa mpenzi wake amepata mpenzi mwingine ambaye pia ni tajiri kama yeye aitwaye Patiyo.

Abesh anamfahamu Patiyo kuwa ni tajiri mwenzake na mara kwa mara huwa wanakutana, kutaniana na kubadilishana mawazo kwenye vikao vyao, pamoja na mikutano ya wafanyabiashara na serikali.

Hakutegemea kama jamaa huyo anaweza kumchukua mpenzi wake, ambaye wameahidiana mambo mengi na wametoka mbali.

Kibaya zaidi akasikia kuwa wiki ijayo mpenzi wake Grace anafunga ndoa na Patiyo na sherehe kubwa itafanyika kwanza kwenye jumba lake la kifahari maeneo ya Kibada, Kigamboni jijini Dar es Salaam, na baadaye kwenye hoteli moja ya kifahari katikati ya jiji la Dar es Salaam majira ya usiku.

Hiyo ni baada ya ndoa kufungwa kwenye kanisa la Mtakatifu Joseph katikati ya jiji la Dar es Salaam.

Hakuwa tayari kuona jambo hilo linafanyika mbele ya macho yake. Linafanyika kwa mtu ambaye ana kila kitu.

Ana pesa, ana ushawishi na kila aina ya zana inayoweza kusababisha anawazuia Grace na Patiyo kuwa mke na mume.

Ndipo alipobuni mpango kabambe wa kuwaangamiza mbele ya macho yake watoweke duniani ili abaki na amani moyoni.

Kwa kutumia pesa zake na ushawishi alitafuta vijana wanne wanaoweza kufanya vitu tofauti, lakini lengo likiwa ni moja tu, Grace na Patiyo watoweke duniani kwa sababu hawana adabu.

Hawawezi kumdhalilisha, kumfedhehesha na kumtia aibu mtu kama yeye ambaye ametunikiwa utajiri, umaarufu na vitu vingine vinavyofanana na hivyo.


Abesh, ndiyo aliyekuwa akiongea na vijana hao ambao tayari wameshapewa maagizo ya nini wanachotakiwa kwenda kufanya.

Watu hao ameletewa na watu wake wa karibu na anaowaamini na kuambiwa kuwa hao ni vijana wenye uwezo wa hali ya juu wa kazi hizo.

Na hata alipozungumza nao na kupanga mikakati, ilionyesha kuwa ni kweli wameiva. Sasa kilichobaki ni kitu kimoja tu kuwamaliza Grace na Patiyo.

*****************************

Anaitwa Tofiki Seif. Alizaliwa Tanga mjini. Baba yake alikuwa ametokea Mombasa nchini Kenya na




**Rafiki zake wa Kiarabu ambao baadhi yao walipokuwa wakubwa walienda kuishinchini Oman, walimletea zawadi ya gari maalum la mashindano na hiyo ikamfanya kuingia kwenye mashindano.**

kuweka makazi yake mjini humo. Alioa mwanamke wa Kidogo na kupata watoto watano, mmoja akiwa Tofiki.

Hakuwa mzuri darasani. Jirani ya nyumbani kwao alikuwa na marafiki zake watoto wa Kiarabu ambao wazazi wao walikuwa wanamiliki malori na magari mengine madogo.

Kucheza na watoto hao wa Kiarabu, kulimfanya awe karibu na magari hayo kwani rafiki zake walikuwa akijifunza wakiwa bado wadodo. Na yeye walimfundisha akiwa na miaka 12 tu. Alifahamu kuendesha gari akiwa mdogo na hata alipofika umri wa miaka 15 tu alikuwa na uwezo mkubwa wa kuendesha lori lenye tela.

Kabla hata hajafika umri wa miaka 18, mwili wake tu ulipojaa kidogo na kuwa na uwezo wa kuwadanganya matrafiki, alianza kazi ya kuendesha malori kwenda kwenye mikoa mingine na hata nje nchi.

Rafiki zake wa Kiarabu ambao baadhi yao walipokuwa wakubwa walienda kuishi nchini Oman, walimletea zawadi ya gari maalum la mashindano na hiyo ikamfanya kuingia kwenye mashindano. Akashinda kwa miaka mitatu mfululizo.

Mmoja kati ya mashabiki wake Haruna, alimfuata na kumwambia kuwa hata kama akiwa na kazi ya kuendesha malori, pia kushiriki mashindano ya magari na kulipwa pesa, lakini anaweza kufa masikini kama hatotumia kipaji chake cha kuendesha gari kwa kasi vizuri. Alimwambia anaweza kupata pesa nyingi kama tu anashirikiana na majambazi kwa ajili ya kuwapeleka eneo la tukio na baada ya hapo kuwakimbiza mara moja kwa sababu ya kipaji chake cha kuendesha gari kwa kasi.

Awali alisita, lakini baadaye akakubali. Alitaka afanye mara moja. Lakini pesa aliyoipata mara ya kwanza ilikuwa nyingi. na uwezo mkubwa alioonyesha uliwafanya majambazi kumpenda na kupeana taarifa, hivyo mara kwa mara alipata tenda. Habari zake za kutambaa na gari ziliwaacha hoi hata askari polisi zilimfanya leo kuwa kwenye kikao kile chini ya Abesh Abdallah. Kazi yake ilikuwa ni kuwapeleka jamaa kwenye eneo la tukio na baada ya hapo kuwaondoa eneo hilo la mauaji haraka na kuwarudisha sehemu salama waliokubaliana kwenda baada ya hapo.

************************************

Jina lake kamili ni Michael Sabuni. Alizaliwa mkoani Iringa na kumaliza shule ya msingi huko huko. Alikuwa hapendi shule kabisa. Na si kupenda tu, lakini pia alikuwa mbabe, akipiga walimu na mara kwa mara alikuwa kwenye hatari ya kufukuzwa shule. Alipomaliza shule ya msingi hakutaka tena mambo hayo.

Kutokana na ukorofi na nguvu alizonazo, alijiingiza kwenye fani ya masumbwi. Nia akitaka kuwa mmoja wa mabondia wazuri na maarufu ili wakoge wote waliokuwa akimcheka kwa sababu hakusoma.

Haikuwa hivyo. Kwani alichoona ni mazoezi magumu, yaliyohitaji uvumilivu wa hali ya juu, huku kukiwa hakuna posho za kutosha wala mishahara. Ukata ukamfanya Michael kukata tamaa. Na hata akienda kupigana, pesa anazolipwa hazikuweza kukidhi mahitaji yake.

Akaamua kujiingiza kwenye uhalifu na kukaba watu na kuiba. Aliifanya kazi hiyo kwa muda mrefu, kabla hajanogewa na kujiingiza moja kwa moja kwenye ujambazi.

Alikuwa na uwezo mkubwa wa kutimia silaha mbalimbali, lakini sifa yake kubwa ilikuwa ni kupiga ngumi, judo na mtaalam kwenye vurumai.

Alikuwa amechukuliwa kwenye mpango huo wa Abesh, kazi yake ikiwa ni kumlinda Tamim akiwa kwenye kazi ya kuua maharusi Grace na Patiyo.

Lengo ni kuhakikisha Tamim anaifanya kazi hiyo vizuri na kwa usahihi, bila kuhofia kitu chochote nyuma, au mtu yoyote kama anamtazama au kumfuatilia.

Sabuni wakati huo anatakiwa kuwa na kamera, ili aonekane ni mmoja kati ya waliopewa tenda ya 'kushuti' video za maharusi, kumbe ni kuhakikisha hakuna mtu yoyote atakayemsumbua Tamim, kumkaribia au kumfuatilia au kumshuku. Yoyote atakayeonekana yoko katika hali hiyo, zawadi yake ni kifo.

Sabuni hakuna na wasiwasi na kazi aliyopewa. Alishakuwa mzoefu na kufanya matukio mengi ya hatari zaidi kuliko hilo.

*************************************

Watoto wa mjini wanamwita Kidaga. Sijui kwa nini. Lakini wazazi wake walimpa jina la Fadhili. Alizaliwa jijini Dar es Salaam. Alisomea na kukua kwenye jiji hilo. Kufahamiana na watu wengi tofauti wanjanja wanjanja wa mjini, kukmfanya kujiingiza kwenye kazi za kijanja, zilizowapatia pesa za haramu kwa muda mfupi.

Alishawahi kufanya kazi ya utapeli wa magari na nyumba na kumpatia pesa nyingi, alizojenga nyumba na kumfanya kuishi maisha ya fahari.

Pia, hakuwa mbali na ujambazi. Alifanya kazi hiyo hasa alipoona kuwa ina fungu kubwa. Kutokana na kuwa ni mtoto wa Dar, alitumika kama ni mchora ramani, na ndiye aliyekuwa akipeleka habari kwa majambazi wenzake ni wapi kuna pesa, nani anapeleka pesa benki na lini. Dili inapofanyika yeye naye hupewa mgao wake.

Kazi nyingine kubwa na kusimamia kazi nzima na kuamrisha nini kifanyike wakati huo, au nini kisifanyike, lakini pia kujua njia, mitaa na maeneo mengi ya Dar es Salaam.

Kwenye operesheni hii alichukuliwa kama msimamizi mkuu. Yeye ndiye mratibu na wakati wa tukio atakuwa amebaki ndani ya gari lenye vioo vya giza akiwasiliana na Michael pamoja na Tamim ambao watakiwa nje wakikamilisha kazi ya kuhakikisha maharusi wanauwa.

Wakati huo, pia Kidaga atakuwa anawasiliana na bosi Abesh kuhusu nini kinaendelea sehemu ya tukio.

**Itaendelea Jumamosi**

# TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA


THE COMPANY ACT CAP 212 (R.E 2002)
RAMCO GROUP LIMITED
(COMPANY NO 126260)

**NOTICE OF RESOLUTION TO WIND UP VOLUNTARILY**

**Notice:** I hereby gave to the general public that by special resolution dated 7/12/2019.

**TAKE NOTICE THAT:** All the creditors are hereby requested to furnish the chairman with full details of their claims against the Company at the address below within 14 days from the date of this notice.

Dated of Dar es Salaam on this 4/3/2020

RAMCO GROUP LTD
P.O BOX 25
MWANZA-TANZANIA.

MAIN MOHAMAD NASSER
CHAIRMAN.

115655202

## KUPOTEA KWA CHETI



**Anna Elieza Mwimbwa** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1231-0007 kilichotolewa na Baraza la mithihani la Taifa mwaka 2017 katika shule ya sekondari Mbabala.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/OST/RB/67181/2020**

156581

## KUPOTEA KWA CHETI



**MOHSIN MSUYA** anatangaza kupotea kwa cheti cha Basic Certificate of Marketing chenye namba **CMK 0000014** kilichotolewa na Chuo cha College of Business Education 2009.

Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/CHA/RB/160286/2019**

115658702

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

## TAARIFA KWA UMMA

Ndugu mwananchi mnatangaiwa tarehe 09/11/2020 kampuni ya **chico (china henan internation cooperation group co.ltd)** itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **DODOMA** kuelekea **MANYONI** kupitia **KIGWE,** gari hilo lenye namba za usajiri **T507 BKM/ 509BKM** ,yenye escort no T304 CVZ

Gari hilo linavipimo vifuatavyo
- Urefu mita 20.00m
- Upana 3.00m
- Kimo 5.00m

Njia itakayo tumika ni **DODOMA** hadi **MANYONI** kupitia **KIGWE**

Gari itasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jion

**Tunaomba radhi kwa usumbufu**

2156594

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA,

## TAARIFA KWA UMMA

Ndugu mwananchi mnatangaiwa tarehe **11/03/2020** kampuni ya chico (china henan internation cooperation group co.ltd) itasafirisha mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka MANYONI kueleakea **DODOMA kupitia KIGWE**, gari hilo lenye namba za usajiri **T507 BKM/ 509BKM** ,yenye escort no **T304 CVZ**

Gari hilo linavipimo vifuatavyo
- Urefu mita 20.00m
- Upana 3.00m
- Kimo 5.00m

Njia itakayo tumika ni **MANYONI hadi DODOMA kupitia KIGWE**

Gari itasafiri muda wa mchana tu kuanzia saa 12:30 asubuhi mpaka saa 12:00 jion

**Tunaomba radhi kwa usumbufu**

2156597

## KUPOTEA KWA CHETI NA RESULT SLIP



**ELISHA ATILYO MKEMWA** anatangaza kupotelewa na Leaving Certificate ya kidato cha nne yenye index namba **NS 0325/0106/2012** iliyotolewa na LUGALO SEKONDARI mwaka 2012 pamoja na Result Slip.

Yeyote atakayeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi:
**UD/BI/I/VOL XI/16/2020.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA
AT DODOMA
PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE
NO.10 OF 2020
In the matter of the Estate of the late
LEONARD USUMBA MADEJE of Muungano
Area within Dodoma Region.**

**AND
IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR
LETTERS OF ADMINISTRATION BY
CLEMENCE LEONARD USUMBA**

**GENERAL CITATION
(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 163)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before 09th day of MARCH 2020.

Date at Dodoma this 5th day of February 2020

RESIDENT MAGISTRATE

RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA REGION

215659502

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAHMA ZUBEIR ABDALLA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 553 ARR Mitsubish Canter. Chassis namba FE537B522304.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
DAR/BUG/RB/206879/2020.


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe
MWANGA WA JAMII


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO




# NEYMAR NJIA NYEUPE KUREJEA BARCELONA

**PARIS,** Ufaransa

MABOSI wa PSG wameripotiwa wapo tayari kumuuza nyota wao Neymar ambaye amekuwa akitakiwa kwa udi na uvumba kurudi Barcelona.

Taarifa kutoka korido za PSG zinaeleza kuwa, Neymar anaonekana kuwa jirani na mlango wa kutokea na kurejea zake Barcelona baada ya uhusiano wa wawili hao kuharibika. Vyombo vya habari vya Hispania vinaeleza kuwa, Neymar bado ana kiu ya kuachana na PSG na kurejea Camp Nou ili kuungana na wachezaji wenzake wa zamani.

Neymar anataka kutumia kuvunjika kwa uhusiano huo kama kigezo cha kulazimisha kuondoka Paris huku wachambuzi wa mambo wakieleza kuwa Barca watalazimika kuvunja benki na kulipa pauni milioni 157 ili kumchukua.

Uhakika zaidi wa Neymar kuachana na PSG utaongezwa nguvu na vipengele kwenye mkataba wake wa sasa ambao, unamruhusu kununua muda uliobaki kwa mujibu wa kanuni za Shirikisho la Soka Duniani, FIFA.

Hata hivyo, kama hilo litatokea basi Neymar atalazimika kupunguza mshahara wake wa sasa hadi pauni 403,000 ili alingane na Messi ambaye ndiye anavuta mzigo mkubwa klabuni hapo.

# Reus aipa pigo Dortmund kuelekea kuivaaa PSG

**DORTMUND,** Ujerumani

KOCHA wa Borussia Dortmund, Lucien Favre, amebakia hana uhakika wakati gani Marco Reus atarudi kutoka majeruhi ya misuli.

Reus alilazimika kutolewa nje wakati kikosi chake cha DFB-Pokal kikipoteza kwa Werder Bremen Februari 2, huku miamba hao wa Bundesliga awali walitangaza asingeweza kurudi kwenye mazoezi kwa wiki nne.

Favre alithibitisha Alhamisi kwamba, fowadi huyo wa Ujerumani anaendelea kujiuguza, na hatakuwapo kwenye mchezo wa Dortmund dhidi ya Borussia Monchengladbach Jumapili.


"Siwezi kuwaambiwa muda gani atarudi. Ameanza mazoezi ya ndani jana (juzi), lakini hayo ndiyo pekee ninayoweza kusema kuhusu hili," alisema Favre akiwaambia waandishi wa habari.

Ufiti wa Reus unaibua aswali mengi kuelekea kwenye mchezo wa marudiano wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 bora dhidi ya Paris Saint-Germain Jumatano ijayo.

Walikuwa bila nahodha wao kwa mara ya kwanza wakati walipokutana kwa mara ya kwanza pale kwenye dimba la Signal Iduna Park, ambapo Erling Haaland alifunga mabao mawili kwenye ushindi wa 2-1 dhidi ya Wafaransa hao.

Huku Reus bado akiwa anajiuguza, Favre anaweza kumchukua Mario Gotze kuziba nafasi yake.





# *Hazard afanyiwa operesheni Marekani*

**DALLAS,** Marekani

EDEN Hazard amefanyiwa operesheni ya mafanikio kwenye enka yake mjini Dallas nchini Marekani.

Nyota huyo wa Real Madrid aliumia enka ya mguu wa kulia wakati wa mchezo wa kipigo cha bao 1-0 wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, kutoka kwa Levante.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 alipelekwa kufanyiwa operesheni hiyo nchini Marekani.

Kwa mujibu wa ripoti za vyombo vya habari vya Hispania, mchezaji huyo alipelekwa Marekani ili kukutana na madaktari wataalamu wa operesheni ambao wanawafanyia nyota wa Ligi Kuu ya mpira wa kikapu ya NBA.

Madrid ilithibitisha juzi Alhamisi kwamba, operesheni ya Hazard ilifanyika kwa mafanikio makubwa kama ilivyopangwa, chini ya uangalizi wa madaktari bingwa, na ataendelea kuwa chini ya uchunguzi kabla ya kuanza mazoezi.

Hazard, ambaye amecheza mechi 15 kwa Madrid tangu alipojiunga kwa euro milioni 100 akitokea Chelsea.

## Maguire shakani kuikabili City

**MANCHESTER,** England

HARRY Maguire yupo shakani kuichezea Manchester United dhidi ya wapinzani wao wa jiji moja, Manchester City, kutokana na maumivu wa enka.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England hakuwapo kwenye kikosi cha United katika mchezo wa raundi ya tano wa Kombe la FA wakati wakishinda dhidi ya Derby County Alhamisi. Ole Gunnar Solskjaer alibainisha kwamba, alipanga kumchezesha nahodha huyo wa United dhidi ya Rams hao kwani ilikuwa ni siku yake ya kumbukumbu ya kuzaliwa akitimiza umri wa miaka 27.

Hata hivyo, majeruhi ya Maguire yamemwacha bosi Solskjaer kutokuwa na uhakika kama atamchezesha beki huyo wa kati dhidi ya kikosi cha Pep Guardiola pale kwenye dimba la Old Trafford.

"Nilikuwa na neno nae kabla ya mazoezi jana (juzi), sitamjaribu kumchezesha dhidi ya Derby," alisema Solskjaer akiiambia MUTV.






## SOLSKJAER APAGAWISHWA NA KIWANGO CHA IGHALO

**LONDON,** England

OLE Gunnar Solskjaer amemsifia Odion Ighalo kwa "kufanya kile kinachosemwa kinawezekana" baada ya kuifungia mabao mawili Manchester United dhidi ya Derby County.

Ighalo alitikisa nyavu mara mbili baada ya bao la ufunguzi la Luke Shaw pale kwenye dimba la Pride Park Alhamisi wakati United wakiibuka na ushindi wa magoli 3-0 kwenye mechi ya raundi ya tano ya Kombe la FA.


Mchezaji huyo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Nigeria alijiunga na United kwa mkopo akitokea Shanghai Shenhua Januari na tayari amefunga mabao matatu katika mechi sita alizocheza.

Solskjaer, ambaye sasa kikosi chake kitacheza na Norwich City kwenye robo fainali ya FA, amesema fowadi huyo alifanya kile kilichotarajiwa.

"Ighalo anafanya kile kinachosemwa kinawezekana. Aliingia na kucheza mbele, tofauti kama mshambuliaji," amesema kocha huyo wa United akiwaambia waandishi wa habari.

"Anapata nafasi katika kila mchezo, leo (juzi) angeweza kuwa na mabao mengine kadhaa. Nina furaha juu yake. Anatupa nafasi wakati Mason (Greenwood) na Anthony (Martial) wanaweza kutulia."

Kuelekea mchezo dhidi ya Manchester City Jumapili, United haijaruhusu bao kwenye mechi zake zilizopita kati ya nne.




## Rooney atumaini vijana kujifunza kwa Man Utd

**LONDON,** England

KOCHA mchezaji, Wayne Rooney, ana matumaini wachezaji wenzake vijana wa Derby County watanufaika kutokana na uzoefu walioupata kwenye mchezo dhidi ya Manchester United wa raundi ya tano ya Kombe la FA.

Derby walifungwa 3-0 pale kwenye dimba la Pride Park Alhamisi, huku Luke Shaw akifunga la kwanza kabla ya Odion Ighalo kufunga mawili na kuipeleka robo fainali na itapambana na Norwich City.

Rooney alikabiria kuifunga klabu yake ya zamani, lakini shuti lake la dhabu ndogo liliokolewa na Sergio Romero.

Hata hivyo, nahodha huyo wa zamani wa United aliungana na wachezaji vijana kama Max Bird (19), Louie Sibley (18) na Jason Knight (19) ambao walionyesha kiwango cha kuvutia.

Sibley alicheza vizuri zaidi kwenye nafasi ya kiungo huku akimpelekesha Scott McTominay. Na Rooney aliridhishwa na kiwango cha kikosi chake, licha ya kupoteza mchezo huo kwa kichapo.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# ARSENAL YAJITOSA KUMWANIA KOKCU

Arteta ajipanga kuwauza 'vimeo' akiwamo Ozil ili kurahisisha mchakato wa kusaini nyota wapya...

**LONDON,** England

KOCHA Mikel Arteta anajiandaa kuwauza wachezaji ambao hawana nafasi za kudumu katika kikosi cha Arsenal katika kipindi cha majira ya joto ili kuruhusu mchakato wa kusajili nyota wapya.

**Arsenal tayari imeshaanza mazungumzo na Feyenoord kwa kuweka dau la pauni milioni 23 ili kuwania saini ya kiungo mchezeshaji wa timu hiyo, Orkun Kokcu na ili kufanikisha mchakato huo, Arteta analazimika kuwaondoa nyota asiowahitaji.**

Matteo Guendouzi, Sokratis na Ainsley Maitland-Niles wamekalia kuti kavu wakati mchezaji ambaye alitajwa mara kadhaa kuuzwa, Mesut Ozil, ataruhusiwa kuondoka klabuni hapo.

Ozil yuko katika kikosi cha Arsenal tangu kipindi cha majira ya joto mwaka 2013 alipotua akitokea Real Madrid na tangu msimu huu ulipoanza, amecheza mechi 22 tu za mashindano yote.

Wakati huo huo, Lucas Torreira alitarajia kukutana na daktari kwa ajili ya kumfanyia uchunguzi baada ya kupata maumivu ya enka katika mechi ya raundi ya tano ya Kombe la FA dhidi ya Portsmouth iliyochezwa Jumatatu iliyopita ambayo kikosi cha Arteta kilipata ushindi.

Arteta anamatumaini kiungo huyo wa Timu ya Taifa ya Uruguayi atarejea kikosini kabla msimu huu haujamalizika.

Katika hatua nyingine, Arteta amekanusha tetesi amefanya mazungumzo na Real Madrid kuhusiana na kumpa mkataba wa kudumu Dani Ceballos.

Nyota huyo ambaye ana umri wa miaka 23 yuko Arsenal kwa mkopo wa muda mrefu akitokea Bernebeu ingawa mkataba wake haukuwa na kipengele kinachowaruhusu kumnunua moja kwa moja.

Ceballos amekuwa katika hali ya sintofahamu kutokana na kuanza msimu akiwa majeruhi na hali hiyo imerejea tena, na inaelezwa kwamba Mhispania huyo alifanya mawasiliano ya kurejea Madrid katika dirisha dogo la Januari mwaka huu.

Ceballos amecheza mechi 23 katika mashindano yote msimu huu akiwa na The Gunners, akifunga bao moja na akitengeneza nafasi mbili za kufunga kwa wachezaji wenzake.

"Hakuna mazungumzo yoyote ambayo yamefanyika," Arteta aliwaambia waandishi wa habari katika mkutano uliofanyika juzi Alhamisi.

## ZISIKUPITE

### MBAPPE KUIKOSA OLIMPIKI

SHIRIKISHO la Soka Ufaransa (FFF), limepokea barua rasmi kutoka kwa Paris St-Germain ikieleza klabu hiyo haitaki straika wake Mfaransa Kylian Mbappe (21), ajumuishwe katika kikosi kitakachokwenda kushiriki Michezo ya Olimpiki mwaka huu nchini Japan. ***(ESPN)***

### DOMINIC KIMEELEWEKA

STRAIKA wa Everton raia wa England, Dominic Calvert-Lewin (22), yuko tayari kusaini mkataba mpya wa muda mrefu na Toffees. Mkataba huo atakaosaini utamweka klabuni hapo hadi mwaka 2025. ***(Times)***

### MAGALHAES KUTUA EVERTON

MABOSI wa Everton wameanza mazungumzo na Lille kwa ajili ya kunasa saini ya beki Mbrazili Gabriel Magalhaes (22), ambaye katika dirisha dogo la usajili la Januari alihusishwa na Arsenal na Tottenham. ***(Independent)***

### IGHALO MAMBO SAFI

STRAIKA wa Manchester United Mnigeria Odion Ighalo (30), ambaye yuko kwa mkopo kutoka katika klabu ya Ligi Kuu China, Shanghai Shenhua, anatarajiwa kupewa mkataba wa kudumu Old Trafford. ***(Mail)***

### CEBALLOS MTEGONI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta amekanusha kufanya mawasiliano na Real Madrid ili kuwania saini ya kiungo wa Timu ya Taifa ya Hispania, Dani Ceballos (23), ambaye anaichezea timu hiyo kwa mkopo ili kupewa mkataba wa kudumu. ***(Marca)***

### CHELSEA YAMWINDA CAKIR

CHELSEA inajiandaa kuwasilisha maombi ya kuwania saini ya golikipa wa Trabzonspor na Timu ya Taifa ya Uturuki, Ugurcan Cakir (23), ambaye pia alihusishwa na kujiunga na Liverpool ili kuchukua mikoba ya Muhispania, Kepa Arrizabalaga (25). ***(Fotospor, via Express)***

### SANCHO AIGOMEA CITY

WINGA wa Timu ya Taifa ya England, Jadon Sancho, amekataa ofa ya kulipwa mshahara wa pauni 30,000 kwa wiki na Manchester City na sasa anataka kujiunga na Borussia Dortmund. ***(Mail)***

### SKIPP, SPURS SAFI

KLABU ya Tottenham iko tayari kumpa ofa ya mkataba mpya kiungo wake aliyekulia klabuni hapo, Oliver Skipp, ambaye ana umri wa miaka 19. ***(Football Insider)***

### DAVID ATAJWA ARSENAL

ARSENAL inajiandaa kufanya mchakato wa kuwania saini ya straika wa Gents na Timu ya Taifa ya Canada, Jonathan David (20). ***(Goal)***

### SANSON ANUKIA EPL

LEICESTER City imetajwa kumwania kiungo wa ld Marseille, Morgan Sanson ambaye ana umri wa miaka 25. ***(Jeunes Footeux, via Leicester Mercury)***

### MOWATT KUBAKI BARNSLEY

KOCHA Mkuu wa Barnsley, Gerhard Struber anaamini kiungo wa zamani wa Timu ya Taifa ya vijana ya England (U-20), Alex Mowatt, ambaye sasa ana umri wa miaka 25, atasaini mkataba mpya na klabu hiyo ndani ya siku chache. ***(Yorkshire Post)***

## HABARI MICHEZO

### Muumin aibukia Shadai Tikisatikisa

**Na Sabato Kasika**

MWANAMUZIKI mkongwe na maarufu wa muziki wa dansi hapa nchini, Mwinjuma Muumin, ameibuka na bendi mpya iitwayo Shadai ambayo itatumia mtindo wa 'Tikisatikisa'.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Muumin, ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Shadai, alisema wakati anaitambulisha bendi hiyo, kuwa tayari wameshaandaa nyimbo tisa. Muumin alizitaja baadhi ya nyimbo ambazo zimeandaliwa na bendi hiyo kuwa ni pamoja na Nimefulia, Maajabu ya Mgongo, Minnie, Ushauri wa Mama, Mwanadamu Haridhiki na Alkasusu.

Alisema bendi hiyo inaundwa na wanamuziki 18 akiwamo mpiga solo wa muda mrefu, Rashid Sumuni, rapa Saulo Ferguson na mpiga besi wa zamani wa bendi ya Akudo, Dekanto.

# MANARA AWATAKA SIMBA KWENDA KUMALIZA UBISHI

**Na Saada Akida**

KUELEKEA mechi ya watani wa jadi, Simba na Yanga itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano ya Simba, Haji Manara, amewataka mashabiki wa klabu hiyo kujitokeza kwa wingi kuwashangilia vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mchezo huo ni wa marudiano katika msimu huu wa mwaka 2019/20 baada ya ule wa kwanza uliochezwa Januari 4, mwaka huu kumalizika kwa sare ya mabao 2-2.

Akizungumza na gazeti hili kutoka Hispania, Manara alisema amezungumza na nahodha wa timu yao, John Bocco na kumuhakikishia kikosi chao kitashuka kupambana kwa lengo la kusaka ushindi.

**Manara alisema kutokana na ahadi hiyo, anawaomba mashabiki wajitokeze uwanjani kuishangilia timu yao yenye uhakika wa kufanya vizuri kwa kuwafunga Yanga.**

"Nimeongea na mabosi wangu, timu ipo vizuri mashabiki naomba sana wajitokeze kwa wingi tuanze kuwafunga kabla ya mechi, wajipange kushangilia lakini pia wekeni akiba ya maneno," alisema Manara.

Aliongeza Simba ni timu kubwa hivyo mashabiki wasijibizane na Yanga na badala yake wakae kimya huku jukumu hilo akijipanga kuwajibu baada ya mechi hiyo kumalizika.



"Kwa mara ya kwanza huenda nikakosa mchezo huo kutokana na majukumu ya kazi, lakini tupo pamoja, mashabiki wajitokeze kushangilia na pia twendeni tu kuchangia mishahara yao, tuwafumue na tujaze uwanja na tuwaambie Afrika timu kubwa Tanzania ni moja, Simba," alisema Manara.



Mwanamuziki Muumin Mwinjuma (katikati), akizungumza kuhusu utambulisho wa bendi mpya iitwayo Shadai itakayozinduliwa Machi 28, mwaka juu jijini Dodoma. Wengine katika picha ni wanamuziki wa bendi hiyo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# *Viongozi wa Simba SC, Yanga watambiana*

**Na Saada Akida**

IKIWA imebakia siku moja kabla vigogo wa soka nchini hawajakutana, Katibu Mkuu wa Yanga, David Ruhago, amesema kikosi chao kimejipanga kuonyesha soka safi na kurejesha furaha klabuni hapo.

Yanga iliyo chini ya Kocha Mkuu, Luc Eymael, itawakaribisha Simba kwenye mchezo wa pili wa Ligi Kuu Bara ikiwa na kumbukumbu ya kutoka sare ya kufungana mabao 2-2, uliochezwa Januari 4, mwaka huu.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ruhago alisema kikosi chao kipo vizuri na tayari kwa ajili ya mchezo huo huku kila mmoja akiamini wanakwenda kuifunga Simba.

Ruhago alisema mashabiki wa Yanga wasihofie kitu chochote kutokana na wachezaji wao wamejiandaa kuondoka na ushindi katika mechi hiyo kwa sababu ya maandalizi bora waliyofanya na morali ya wachezaji wao kuwa juu.

" Mashabiki wa Yanga Jumapili ni siku yetu kuonyesha soka lisilo na makandokando, kila mchezaji anajua jukumu lake, tupo tayari kuonyesha soka safi kwa kuwa tumejipanga na tunaamini inawekezekana," alisema Ruhago.

Naye, Kaimu Katibu Mkuu wa Simba, Hamisi Kisiwa, amesema kikosi chao hakitaingia uwanjani na matokeo kichwani lakini wamejiandaa kupambana kusaka ushindi katika mchezo huo muhimu dhidi ya Yanga.

"Niwaombe mashabiki wa Simba wajitokeze, kwa upande wetu hatutaingia uwanjani na matokeo, bali tutaingia uwanjani kutafuta matokeo mazuri," alisema Kisiwa.

Alisema kocha wao amefanyia kazi upungufu wa kikosi hicho ili kutorudia makosa yaliyojitokeza katika mchezo uliopita kwa malengo ya kumpa furaha Rais wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF) Ahmad Ahmad, ambaye atashuhudia mechi hiyo.

### Cannavaro atoa angalizo Yanga

**Na Shufaa Lyimo**

ALIYEKUWA nahodha na beki tegemeo wa Yanga, Nadir Haroub 'Cannavaro' amesema mechi za watani huwa hazitabiriki, lakini anaitakia ushindi timu yake katika mchezo huo utakaowakutanisha dhidi ya Simba kesho kwenye Uwanja wa Taifa.

Cannavaro aliliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, mechi hiyo itakuwa na ushindani kama michezo mingine ya ligi iliyopita lakini anaamini wachezaji wa Yanga wakiongeza utulivu, wataibuka na pointi tatu muhimu.

"Zinapokutana Simba na Yanga, mchezo huo huwa hautabiriki, kwanza ni mechi ngumu ila kwa usajili walioufanya Jangwani, uwezo wa kushinda upo, endapo watajipanga vizuri," alisema Cannavaro.

Beki huyo aliwataka mashabiki wa Yanga kushirikiana kuiombea timu yao ili iweze kutoka na ushindi dhidi ya vinara na mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Yanga itashuka uwanjani kesho ikiwa na kumbukumbu ya kushinda mechi zake mbili zilizopita dhidi ya Alliance FC na Mbao FC, zote kutoka jijini Mwanza.

Nyota wa Yanga waliofunga mabao ya kusawazisha katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Januari 4, mwaka huu ni Mapinduzi Balama na Mohammed Issa 'Banka'.

Michezo

Jumamosi Machi 7, 2020

Nipashe



Neymar njia nyeupe kurejea Barca UKURASA 28



MOLINGA MIQUISSONE

## Azam kuendelea ‘kuitesa’ Alliance

**Na Mwandishi Wetu**

BAADA ya kupoteza mechi yake dhidi ya Simba, mabingwa watetezi wa Kombe la FA, Azam FC, wanatarajia kuwakaribisha Alliance FC kutoka Mwanza katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam.

Hata hivyo Azam FC itashuka uwanjani ikiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 5-0 walioupata dhidi ya Alliance katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini Mwanza.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nahodha wa Azam FC, Aggrey Morris, alisema watarejea uwanjani leo wakiwa na ‘hasira’ baada ya kupoteza mechi iliyopita.

Morris alisema anawaomba mashabiki wao wasikate tamaa kwa sababu ligi ni ngumu na wao wataendelea kupambana hadi mwisho wa msimu.

“Tunapenda kuwaambia mashabiki wetu waendelee kutuunga mkono, tulifanya makosa katika mechi iliyopita na wenzetu Simba wakatuadhimu, tunawategemea sana,” alisema beki huyo.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Singida United dhidi ya Prisons, Ruvu Shooting vs JKT Tanzania, Polisi Tanzania vs Namungo FC, Coastal Union vs Ndanda, Mtibwa Sugar vs Kagera Sugar, Lipuli vs Biashara United, Mwadui vs Mbeya City na KMC itaikaribisha Mbao FC.

# Simba, Yanga zasubiri muda

## Kila upande watamba kuimarika na kutorudia makosa, Rais wa CAF awasili kujionea mtanange huo...

**Na Somoe Ng’itu**

UBISHI, tambo na majigambo mbalimbali yaliyokuwa yakiendelea kutoka kwa watani wa jadi nchini, Simba na Yanga, vinatarajiwa kumalizika katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa kesho jioni kwenye Uwanja wa Taifa jijini Dar es Salaam.

**Mechi hiyo ni ya mzunguko wa pili msimu huu wa 2019/20 baada ya mchezo wa kwanza uliochezwa Januari 4, mwaka huu kumalizika kwa sare ya magoli 2-2, Simba ikitangulia kufunga katika kipindi cha kwanza na Yanga wakasawazisha kwenye kipindi cha pili.**

Simba yenye pointi 68 na ndio vinara na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, watashuka uwanjani wakiwa na kumbukumbu ya kupata ushindi wa mechi tano mfululizo wakati Yanga ilitoka sare michezo mitatu na ikishinda miwili ina pointi 47 na kwenye msimamo wako katika nafasi ya tatu.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Msaidizi na kiungo wa zamani wa Simba, Selemani Matola, aliliambia gazeti hili wamejipamba vema kuhakikisha wanaendeleza ‘dozi’ katika ligi hiyo huku wakiongeza umakini.

Matola alisema wanafahamu mechi hiyo itakuwa na ushindani na changamoto mbalimbali, lakini kamwe hawatarudia makosa yaliyojitokeza katika mechi iliyopita.

“Mechi hizi ni ngumu, lakini ni nyepesi vile vile, tutaingia na mipango na mikakati tofauti na mechi ya kwanza, tunajua Yanga hii si ile tuliyokutana nayo, pia tumejiimarisha kila idara na ninaamini mashabiki wetu watafurahi,” alisema Matola.

Nahodha wa Simba, John Bocco, amesema wachezaji wa timu hiyo wamejipanga kuonyesha ubora wao katika mechi hiyo ili kufikia malengo waliyojiwekea.

“Hatutaki kusema lolote, tunataka kuonyesha vitendo, hatutaki kuahidi lolote lakini tutathibitisha tunachokiamini,” Bocco alisema kwa kifupi.

Naye Kocha Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, alisema wamejiandaa kufanya mashambulizi na kucheza kwa kasi ili kuwadhibiti wapinzani wao Simba wasipate bao.

Hata hivyo Mbelgiji huyo alisema wataivaa Simba kwa tahadhari kutokana na wachezaji wake kuwa wa kiwango cha juu na wenye uzoefu.

Alisema atahitaji kuona wachezaji wake wanafuata maelekezo aliyowapa na hilo likifanyika anaamini pointi tatu zitakuwa za Jangwani.

“Tunakwenda kupambana, na kwa uwezo wa Mungu tutafanya mapambano ya kweli na tutaonyesha soka safi,” Juma Abdul nahodha na beki mzoefu wa Yanga alisema.

**AHMAD AWASILI NCHINI**

Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), limeandaa mapokezi ya heshima kwa Rais wa Shirikisho la Afrika, (CAF), Ahmad Ahmad, ambaye anatarajiwa kuwasili nchini leo na ndiye mgeni rasmi kwenye mchezo wa watani wa jadi.

Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema Ahmad atakuwa nchini kwa ziara maalumu ya siku tatu.

Ahmad anakuja nchini kutazama mechi hiyo baada ya kuomba mwaliko kwa Rais wa TFF, Wallace Karia, kutokana na kupata taarifa za mechi za watani zinavyokuwa na burudani na ushindani ndani na nje ya uwanja.

Refa Martin Saanya anatarajiwa kuchezesha mechi hiyo akisaidiwa na waamuzi wengine watano ambao ni Mohammed Mkono, Frank Komba, Elly Sasii, Abdallah Mwinyimkuu na Ramadhani Kayoko huku Kamisaa akiwa ni Mohammed Mkweche.

Wakati huo huo aliyekuwa Mfadhili wa Simba, Azim Dewji, ameahidi kutoa tiketi 300 za kushuhudia mtangane huo kwa mashabiki watakaokwenda kutoa damu katika Hospitali ya Rufaa ya Muhimbili ili kuchangia wahanga wa ajali.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >